SUPA JACKPOT
TZS. 1,033,283,276
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO
CHADEMA

**CHADEMA, TLS wamulika vizuizi vya Katiba Mpya**
UKURASA 2



UKURASA 9

Nipashe
Jumapili Septemba 25, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581079
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Polisi: Kama umeibiwa njoo uchukue mali zako

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### MGOGORO WA NCCR WAHAMIA TAKUKURU

MKUTANO Mkuu wa Dharura wa chama cha NCCR- Mageuzi umeamua wanaotuhumiwa kufanya ubadhirifu wa mali za chama, wafikishwe katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)...

UKURASA WA 5

### WATU 33,000 WAFA KILA MWEZI KISA MOSHI WA KUNI

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amesema moshi wa kuni za kupikia unaua watu 33,000 kwa mwezi kutokana na kutengeneza sumu inayoua taratibu huku ukichangia kuharibika kwa mimba...



Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Awadhi Haji (wa pili kushoto), akionyesha kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, baadhi ya televisheni zilizokamatwa kwa watuhumiwa maarufu kama 'Panya road' katika msako unaoendelea. Picha ndogo: Kamishna Awadhi, akionyesha moja ya mikasi mikubwa wanayotumia kuvunjia milango na kukatia nondo za madirisha. Kushoto ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali yapata mbinu kuzuia mauaji

UKURASA 2



RIPOTI MAALUM

## Hatari iliyojificha kwa uchokonoaji masikio

UKURASA 4

MICHEZO CAG AANIKA UBADHIRIFU UWANJA WA AMAAN, Z'BAR UK.23 MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekarage (kulia), akiangalia watoto njiti waliohifadhiwa kwenye vifaa maalum vilivyotolewa kwa msaada na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Ifakara, katika Hospitali ya Rufani ya Temeke, mkoani Dar es Salaam jana, alipokuwa akikagua utekelezaji wa Programu ya Nest 360, inayosimamiwa na taasisi hiyo. Kushoto ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Joseph Kimaro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA, TLS wamulika vizuizi vya Katiba Mpya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WADAU wa sheria kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), wamedai mchakato wa kupata Katiba Mpya ulioanzishwa mwaka 2011 ulikwamishwa na Bunge Maalum lilioundwa kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo na Tume Maalumu ya Kukusanya Maoni ya Wananchi kwa kuwa wajumbe wake waliteuliwa na Rais badala ya wananchi.

Vilevile, wabobezi hao wa sheria wamedai mchakato wa kupata katiba hiyo pia ulikwamishwa na kile walichokiita udhaifu wa kanuni na utaratibu uliokuwa ukisimamia mchakato huo.

Akizungumza jana Jijini Arusha katika mdahalo wa wazi ulioandaliwa na TLS, mchokoza mada wa kwanza kutoka chama hicho, Wakili Beatus Malima alisema, bunge hilo na tume iliyoundwa zilikwamisha mchakato huo kwa kuwa pande zote hizo ziliangalia maslahi yake badala ya wananchi.

"Kwa uelewa wangu, mchakato ulikwama kutokana na udhaifu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na ile Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2013 pamoja Bunge Maalum na Tume Maalumu ya Kukusanya Maoni ya Wananchi," alidai.

Wakili huyo alidai wabunge hao na wajumbe wa tume hiyo walishindwa kukamilisha kazi hiyo kwa kuwa walikuwa wameteuliwa na Rais na siyo wananchi, hivyo hawakufanikisha kazi hiyo kufikia tamati kwa maslahi yao binafsi.

"Bunge lile liliingilia mawazo ya wananchi kupitia tume iliyokusanya maoni hayo, pia sheria ilitakiwa kuweka kanuni na utaratibu kuwapo kwa bunge hilo na Rais asipewe nguvu ya kuwateua wajumbe hao.

"Pia sheria ingetakiwa kuelekeza utaratibu wa wananchi kuwa wahusika na wenye mamlaka ya kuwachagua wabunge na wajumbe wa tume hiyo watakaokwenda kusimamia jukumu hilo badala ya Rais," alifafanua hoja yake.

Wakili Malima, alisema TLS wana wajibu wa kutoa maoni ambayo yatasaidia kupatikana kwa katiba inayohitajika na wananchi wa Tanzania.

Wakili Dk Rugemeleza Nshala alisema: "Kama katiba itatungwa na isiwe ya wananchi itakuwa ni ya kilema na haiwezi kutibu majeraha ya watu na bunge linaweza kutunga lakini wananchi wakaikataa kwa kuwa kulikuwa na matatizo makubwa katika mchakato ule wa mwaka 2011."

Wakili Iddi Mandi alisema, kazi ya kuandika katiba ni ya kitaalamu na siyo siasa ya kutafuta madaraka, akisisitiza inahitaji kusikiliza watu wanataka nini.

Dk. Elifuraha Laltaika, Mhadhiri Mwandamizi wa Sheria kutoka Chuo cha Tumaini cha Makumira, alidai katika bunge hilo, wabunge waliangalia maslahi yao binafsi ya muda mfupi badala ya Watanzania, akishauri mchakato wa katiba hiyo uendele pale alipoishia Jaji Joseph Warioba kupiga kura na kuandikwa kwa katiba hiyo.

Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA, John Mnyika, alisema Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2013 zina upungufu ambao ulichangia kukwamisha mchakato huo.

Alisema, chama hicho kupitia sheria hizo waliainisha bungeni mambo mbalimbali yaliyotarajiwa kujitokeza kwenye bunge hilo maalum kwa kuwa lilikuwa na idadi kubwa ya wabunge kutoka chama kimoja.

"Kama taifa tunatakiwa sasa tukae na kuandaa sheria mpya za mchakato wa katiba zitakazosaidia kuondoa upungufu wote uliojitokeza huko mwanzo," alisema.

Akifungua mkutano huo, Rais wa TLS, Dk. Edward Hosea, aliwataka washiriki hao kutosahau mambo ambayo yalisababisha kukwama kwa shughuli hiyo na kushauri njia sahihi ambayo itasaidia kupata katiba.

"Chama chetu kinatambua mchango mkubwa unaofanywa na serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika dhamira ya kuhakikisha kunakuwapo utawala bora wa kisheria na kukuza demokrasia nchini," alisema.

# Mgogoro wa NCCR wahamia TAKUKURU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO Mkuu wa Dharura wa chama cha NCCR- Mageuzi, umeamua wanaotuhumiwa kufanya ubadhirifu wa mali za chama, wafikishwe katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Vilevile, mkutano huo umeazimia kumfukuza uanachama Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia na kumvua madaraka Makamu Mwenyekiti, Angelina Mutahiwa.

Katika mkutano huo ulifanyika jana jijini hapa ukihudhuriwa na wajumbe 232 kati ya 368, Wakili Hassan Luhanywa, aliwaambia wajumbe kuwa viongozi waliovuliwa madaraka, wanadaiwa kuteua viongozi kinyume cha utaratibu kwa kukiuka katiba ya chama.

"Madai mengine ni kuwafukuza makatibu wakuu wa chama, kushindwa kulinda na kufanya ubadhirifu na ufujaji wa mali za chama na kujihusisha na migogoro ndani ya chama," alisema. Alisema, mashtaka mengine ya Mbatia ni kushindwa kufanya kazi ya uhamasishaji wa chama na kuwa, msimamo wenye shaka katika kukipenda chama na kulinda mali za chama.

Akidai, Angelina anakabiliwa na mashtaka ya kushindwa kutekeleza majukumu yake na kuanzisha pamoja na kujihusisha na migogoro ndani ya chama.

Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini la chama hicho, Joseph Selasini alisema Halmashauri Kuu ya chama hicho iliyoketi jijini hapa jana iliwafukuza wanachama 11 kwa utovu wa nidhamu uliokithiri. Alidai, wanachama hao walifanya vurugu katika ofisi za NCCR-Mageuzi jijini Dar es Salaam na kutukana viongozi katika mitandao ya jamii.

Aliwataja waliofukuzwa uanachama ni Edward Simbeye, Hemed Msabaha, Mustapher Muro, Nicholaus Clington, Thom Nguma, Joachim Mahega, Victor Ndibalema na Peterson Mshenyera.

Kwa Zanzibar ni Asha Muhsin Ali, Sabikha Mohammed na Salma Mohammed Othman.

Mwenyekiti huyo alisema mkutano huo ulithibitisha aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Haji Ambari Hamis kuwa mwenyekiti wa chama hicho.

## Serikali yapata mbinu kuzuia mauaji nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua Mpango Kabambe wa Afua za Ustawi wa jamii (CCSWOP) huku ikiweka msisitizo kwenye utatuzi wa masuala mbalimbali kwenye jamii ikiwamo matukio ya mauaji ya kujiua.

Mpango huo umeandaliwa kupitia mradi wa Achieve unaotekelezwa na Shirika la Pact Tanzania na mradi wa CHSSP unaotekelezwa na Shirika la JSI kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

Akizindua mpango huo unaoratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, asiye na Wizara Maalum, Kapteni Mstaafu George Mkuchika, alisema jijini hapa juzi kuwa mwongozo huo unapaswa kusimamiwa kikamilifu kwenye utatuzi wa tatizo hilo.

"Mwongozo usimamiwe kikamilifu ili kuwezesha utatuzi wa shida mbalimbali zinazoikumba jamii ikiwamo ukatili wa kijinsia, hasa wanawake na watoto, mauaji na matukio ya kujiua kwa jamii na ongezeko la watoto wa mitaani," alisema.

Alisema mwongozo huo ni muhimu na utasaidia ukusanyaji takwimu na upangaji bajeti za afua hizo.

Alisisitiza usimamizi na utekelezaji wa mwongozo kwa wizara za kisekta huku akiitaka Wizara ya Katiba na Sheria ihakikishe inasimamia urasimishwaji na utekelezaji wa mwongozo.

Pia aliagiza sekretarieti za mikoa zitekeleze jukumu la msingi la kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukusanya takwimu na kuandaa mipango na bajeti za ustawi wa jamii kwa mujibu wa mwongozo huo.

Aliwaomba wadau wa maendeleo nchini kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali kwa kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini. Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Dk. Dorothy Gwajima alisema mwongozo unalenga kuimarisha utoaji huduma kwa makundi maalum ikiwamo wazee, walemavu, watu wenye magonjwa sugu, watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi na makundi mengine.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri alisema kwa miaka sita sasa wamekuwa wakishirikiana na Tanzania kutengeneza mpango huo ambao utaongeza na uratibu wa huduma za ustawi wa jamii.

Alisema mwongozo huo utaongeza ujumuishaji wa huduma kwa makundi maalum na kuchochea mbinu yakinifu katika kukabiliana na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Mkurugenzi Mkazi wa Pact Tanzania, Levina Kikoyo alisema mchakato wa kukamilisha mpango huo umegharimu Sh. milioni 920.1 huku tathmini waliyofanya kwenye halmashauri ambazo zimeanza kutekeleza, imeonyesha mabadiliko makubwa katika utengaji wa bajeti.



Ofisa Programu wa Kitengo cha Jinsia, Watoto, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hakeem Nyangarika (kushoto), akitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa mlemavu Protas Kitoa, Mjini Mpanda mkoani Rukwa, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilichojificha migogoro ardhi chawekwa bayana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TIMU maalumu iliyoandaliwa na serikali kushughulikia migogoro ya ardhi nchini imepokea malalamiko 380 kwa Mkoa wa Dar es Salaam huku ikitenga siku tano kwa Jiji la Dodoma kushughulikia malalamiko ya aina hiyo.

Vilevile, timu hiyo imebaini mambo sita yanayochangia migogoro ya ardhi ikiwamo wananchi kutelekeza maeneo kwa muda mrefu na kutofuata masharti waliyopewa ya umiliki.

Kutokana na hali hiyo, serikali imepanga kuanza operesheni ya kubaini maeneo yote ambayo yamekiuka masharti ya uwekezaji ili wale walioshindwa wanyang'anywe.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, alisema kutokana na kuwapo malalamiko ya migogoro hiyo nchini, wamekuja na utaratibu huo wa kufika mikoa yote na wameanza na Dar es Salaam.

Alisema, timu hiyo inaundwa na wataalamu mbalimbali kutoka Wizara ya Ardhi, mkoa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Rais - Ikulu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na idara zingine za serikali.

"Tumeona haja ya kuwa na utaratibu maalumu wa kushughulikia malalamiko haya badala ya kusubiri mpaka mwananchi mmoja mmoja aje ofisini, tumeona kwamba ni vizuri kuweka utaratibu wa kutembea kwenye mikoa yote nchini ili kusikiliza na kuchambua na kutoa uamuzi kwenye malalamiko ya wananchi kuhusu masuala ya migogoro ya ardhi," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Dar es Salaam wamepokea malalamiko yasiyopungua 380 ambayo yamefanyiwa kazi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi.

**KIINI CHA MIGOGORO**

Alipoulizwa walichobaini kuwa kiini cha migogoro, alibainisha kuwa ni uelewa mdogo wa sheria na kuwapo wajanja wanaotumia sheria kuwadhulumu wananchi ambao hawafahamu sheria na taratibu.

"Wajanja wachache kuuza maeneo ya watu wengine bila kufuata taratibu, wapo madalali wadanganyifu wanauza maeneo ambayo si ya kwao, pia yapo makosa ya kiutendaji kwa watendaji wa serikali wa TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, kuna uamuzi unatolewa na kusababisha mgongano kwa jamii.

"Tunaandaa mwongozo wa taratibu za utawala bora katika mfumo mzima wa uamuzi unaohusu masuala ya ardhi ili watendaji wasio waadilifu wabainike mapema na hatua zichukuliwe kabla migogoro haijawa mikubwa," alifafanua.

Alitaja kiini kingine ni wananchi kutelekeza maeneo kwa muda mrefu na kutofuata masharti waliyopewa ya umiliki na hivyo kuchangia migogoro hiyo.

"Kuna watu wananunua mashamba, viwanja wanatelekeza kwa miaka mitatu, minne mwingine hadi 10, mwingine unafuatilia unamuuliza 'hivi eneo lako lipo wapi?', hata yeye hafahamu.

"Utaratibu ni kwamba ukipewa hati, unapaswa kuendeleza ndani ya miaka mitatu eneo au kiwanja kinatelekezwa, watu wanazunguka wajanja wanakiuza wewe unajitokeza baada ya miaka mitano unasema kiwanja chako na kweli chako lakini umetelekeza, hujaendeleza mtu kaja kaendeleza, hapo ndipo migogoro inaanza," alisema.

Katibu Mkuu alisema siku za karibuni wataanza operesheni ya kubaini maeneo yote ambayo yamekiuka masharti ya uwekezaji ili wale walioshindwa wanyang'anywe kwa kuwa wanasababisha migogoro isiyo ya lazima.

Dk. Kijazi alisema wizara imejipanga kuitafutia ufumbuzi mianya yote inayosababisha migogoro.

**RATIBA YA DODOMA**

Alisema timu hiyo itapiga kambi Dodoma kwa siku tano kuanzia kesho, Jumatatu saa mbili asubuhi hadi saa 10 jioni kwenye vituo vilivyopangwa vya kupokea, kuchambua na kutoa uamuzi kuhusu malalamiko hayo.

"Malalamiko yanayofanyiwa kazi ni yale ambayo hayajafikishwa vyombo vya kisheria na tutatoa mrejesho kwa wananchi kwa maandishi maana changamoto kubwa tunayokabiliana nayo ni wananchi kutopewa mrejesho wa maandishi pale wanaposikilizwa.

"Ratiba ya Dodoma itaanza Septemba 26 hadi 30 mwaka huu, ambapo Mkonze itakuwa Septemba 26 na kuanzia saa mbili asubuhi hadi 10 jioni tutakutana ofisi ya Kata ya Mkonze.

"Septemba 27 timu yetu itakuwa eneo la Kikuyu Kusini na Kaskazini na kituo kitakuwa Ofisi ya Kikuyu Kusini, Ipagala na Makole ni Septemba 28, tutapokea Ofisi za Manispaa ya zamani.

"Kwa wananchi wa Makulu na Iyumbu wafike ofisi za Kata Makulu Septemba 29 na kituo cha mwisho Nzuguni, Mtumba na Kikombo Septemba 30 kituo kitakuwa ofisi za Kata ya Nzuguni," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wa Dodoma na wale wenye maeneo Dodoma yenye migogoro kukutana na timu hiyo.

"Tunataka kila mwananchi apate haki yake kama kuna shida ambazo zimejitokeza kutokana na mifumo ya utendaji tutazitafutia ufumbuzi na kufikia njia mwafaka ya kumaliza migogoro na kama kuna kero zimesababishwa na wananchi wenyewe kwa wenyewe kutokukubaliana kuhusu migogoro iliyopo tutakutana nao na kufikia suluhu," alisema.

Pamoja na hayo, Katibu Mkuu alisema wizara imeongeza kasi ya utoaji wa hati katika mikoa yote.

"Mwananchi yeyote anayetaka hati atapata huduma ndani ya siku moja, suala la kufuata utaratibu ni muhimu ili kupunguza migogoro," alisema.

# Polisi: Kama umeibiwa njoo uchukue mali yako

**Na Romana Mallya**

MSAKO wa wahalifu wanaovunja nyumba usiku mkoani Dar es Salaam na kujeruhi watu kisha kuiba, umewatia mbaroni watuhumiwa 167 huku Jeshi la Polisi likitangaza kukamata silaha za jadi na mali zilizoibwa.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo nchini, CP Awadhi Haji, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu operesheni hiyo huku akiwataka walioibiwa kujitokeza vituo vya polisi ili kutambua mali zao.

"Wananchi walioibiwa mali zao wajitokeze kwenye vituo vya polisi ili kutambua mali hizo, vituo hivyo ni Buguruni, Stakishari, Chang'ombe, Mbagala, Kawe na Kimara," alisema.

Akizungumzia uhalifu huo, Haji alisema unahusisha watu wenye umri kati ya miaka 14 hadi 30 na wamekuwa katika makundi ya watu 10 mpaka 30, wakitumia silaha za jadi, mapanga, visu na nondo kujeruhi na kupora mali.

"Watuhumiwa hao wamegawanyika katika makundi, kuna kundi la wahalifu wanaoshiriki moja kwa moja kuvunja na kufanya uporaji na kundi lingine linalopokea na kununua mali za wizi," alisema.

Haji alisema katika operesheni hiyo wamekamata televisheni (flat screen) 23, redio (subwoofer) mbili, kompyuta (desktop) mbili na spika mbili za sabufa.

Alisema baadhi ya watuhumiwa waliokamatwa, wamekutwa na mapanga 19, vifaa vya kuvunjia, mikasi minne, nondo saba na jeki mbili.

"Tumekamata magari matatu aina ya Toyota Carina yenye namba za usajili T 314 BVY, Toyota Noah T 218 BYS, Toyora Noah T260 BEP na pikipiki tano namba zake ni MC 913 DEH, Boxer MC 405 CVM, MC 856 DFY, MC 206 DDF na moja isiyo na namba," alisema.

Haji alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakitumia pikipiki hizo kubeba zana za kufanyia uhalifu pamoja na kusafirisha mali baada ya uporaji.

Pia, alisema watuhumiwa hao wamekutwa na dawa za kulevya aina ya heroine gramu 35, bangi kilo 63.6 na mirungi yenye uzito wa kilo 9.3.

Alisema, operesheni hiyo ni endelevu na inafanyika nchi nzima ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu.

"Tunatoa tahadhari na onyo kali watu wote wanaojihusisha na vitendo vya kiuhalifu kwa namna moja au nyingine, waache mara moja, Jeshi la Polisi halitasita kuchukua hatua kali.

"Jeshi la Polisi halitasita kuwachukulia hatua za kisheria wazazi au walezi wanawaficha, kuwakumbatia watoto wao wanaojihusisha na matukio ya kiuhalifu ya unyang'anyi na wizi," alionya.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa sahihi ili hatua stahiki zichukuliwe kabla ya vitendo kutokea.

Wiki iliyopita Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam lilitangaza kuwakamata watuhumiwa 116 wakiwa na silaha mbalimbali za jadi.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo baada ya tukio la vikundi hivyo kuvamia kata tatu za Mianzini, Chamazi na Kilungule Septemba 12 na 13, alisema zaidi ya watuhumiwa wa uhalifu 100, wakiwamo wa vijana wa 'panya road' walikamatwa.

Kikundi cha panya road kiliibuka mwezi Aprili mwaka huu na kufanya matukio katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam yakiwamo Chanika, Kitunda, Tabata, Mbezi, Kinyerezi na Kunduchi.


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**FORM NO 58**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 98 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: JAPHET BAINAOMUGISHA KAHEMBE BY 1. GRAYSON BONIFACE KAHEMBE**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 10 day of OCTOBER.........2022

Dated at DAR ES SALAAM this 20 day of SEPTEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi Na 67/ 2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RAJABU MOHAMED WA KAMBAYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KIDAWA RAJABU MOHAMED**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 6 mwezi 10 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Imetolewa leo tarehe 23 mwezi 9 mwaka 2020**

RIPOTI MAALUM

# Hatari iliyojificha dhidi ya wanaochokonoa masikio

Na Romana Mallya



"NILIKUWA na tatizo la kuwashwa masikio kila mara na ili yaweze kutulia, niliingiza kitu chochote chenye ncha sikioni ili kuondoa mwasho, sikujua madhara yake hadi pale masikio yalipoanza kutoa usaha na kwenda hospitalini," Petro Stanslaus, mkazi wa Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam anasimulia mkasa uliotikisa afya yake mwaka jana.

Stanslaus, anayezungumza kwa sauti ya chini na umakini mkubwa, anasema masikio yake yalipopatwa na mwasho, alilazimika kutumia pamba za masikio kujichokonoa ili kupata nafuu na alipokosa, alitumia karatasi, kijiti, njiti za kibiriti, mrija wa kalamu au mfuniko wake na ufunguo.

Kijana Stanslaus, anasimulia zaidi: "Nilifanya hivyo kwa muda mrefu na nilianza kuona usaha ukitoka ndipo nilipokwenda hospitalini na kubaini ule mwasho ulikuwa ukisababishwa na uzio.

"Matibabu ya kutokwa usaha hadi kupona yalichukua zaidi ya miezi mitatu na yaligharimu kwa kweli! Niliambiwa kilichosababisha usaha ni kitendo cha kuweka vitu masikioni, kumbe haitakiwi, nilikuwa sifahamu hilo."

Madhila yaliyomkumba kijana huyo yana ushuhuda mwingine unaofanana kutoka kwa Halima Ramadhani, mkazi wa Temeke mkoani Dar es Salaam anayekiri kuchokonoa masikio yake mara kwa mara anapohisi mwasho, akitumia vifaa vyenye sura ya mtangulizi wake.

"Sifahamu kama kuna madhara ya kuingiza kitu sikioni, nikijikuna napata nafuu, ninaona ni namna ya kulisafisha maana nikiingiza kitu kunatoka uchafu, ila kuna wakati ninahisi kama sisikii vizuri, sijaenda hospitalini kujua tatizo," Halima anasema.

Nipashe Jumapili, inatua mezani kwa Daktari Bingwa wa Upasuaji Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Mlongazila), Godlove Mfuko, anayeonya vikali tabia ya kuingiza vitu sikioni kuwa ni moja ya vyanzo vya matatizo ya masikio.

Dk. Mfuko ana ufafanuzi kwamba mtu anapoingiza pamba sikioni, badala ya kutibu huliongeza tatizo zaidi na husababisha kutosikia au masikio kupiga kelele.

"Mtu mzima anakuja hospitalini pamba imekaa sikioni miezi mitatu. Labda niseme watu maarufu wenye tabia ya kuingiza vitu sikioni ni wanawake, sijui ni mambo ya urembo wanadanganywa wasafishe masikio.

"Kwenye kliniki yangu nikiona wagonjwa wenye shida za masikio zilizosababishwa na kuweka vitu sikioni, kati ya wagonjwa 10, unakuta wanawake ni saba au wanane," anabainisha.

Nini kifanyike? Dk. Mfuko anashauri elimu itolewe zaidi kuhakikisha jamii inatambua kwamba nta inayokaa kwenye sikio siyo uchafu, bali ni ulinzi wa sikio.

"Mtu anakwenda saluni anaoshwa mwili, anawekwa pamba sikioni, hii inaleta madhara zaidi, nta ikiwa nje ya sikio haitakiwi kuguswa, hata ukiilamba ina uchungu, ule uchungu ni dawa ambayo inatengenezwa na ngozi ya sehemu ya nje ya sikio.

"Tunapokwenda kwenye mafunzo kwa vitendo, tumegundua tatizo la usikivu ni kubwa. Mfano, nilikwenda Kigoma, wagonjwa niliowaona, takriban asilimia 26 kati ya wagonjwa 100 waliokuja kwa matatizo ya sikio, pua na koo, walikuwa na shida ya masikio.

"Walikuwa na matatizo ambayo yanahitaji kuingiliwa kati ili kumsaidia mgonjwa, maeneo mengine ni kati ya asilimia 10 mpaka 20," mtaalamu huyo anabainisha.

Dk. Mfuko anasema utafiti wa kuangalia hali ya usikivu kwa watoto uliofanyika hivi karibuni nchini, unaonyesha tatizo hilo lipo kwa asilimia 7.1 na sababu ilikuwa ni nta nyingi sikioni.

"Hapo mzazi ndipo anatumia ufundi wake anaingiza vitu sikioni kuitoa, hii inatakiwa kutolewa kwa utaalamu kwa sababu urefu wa mfereji wa sikio kutoka sikio la nje hadi sikio la kati kwenye ngoma, ni sentimita mbili na nusu. Tuache kuingiza vitu sikioni," anatahadharisha.

Dk. Mfuko anafafanua umuhimu wa nta kwenye sikio, akisema inakamata uchafu wote unaotaka kuingia kwenye sikio na ina dawa ya kuua vijidudu.

Anataja athari za kuingiza vitu sikioni ikiwamo pamba mara kwa mara, huisokomeza nta ndani zaidi wakati imeumbwa kuwa sehemu ya nje ya sikio.

"Nta inakwenda hujikusanya ndani mpaka ikajaa, inapojaa ndipo mtu anakuja hospitalini na tatizo la maumivu, shida ya kengele ya muda mfupi kwenye masikio au tatizo la usikivu," anasema.

Anataja athari zingine ni kuharibu mfumo wa kawaida wa sikio kujisafisha lenyewe, akisema: "Sehemu ya sikio kuna ngozi inatembea kutoka kwenye ngoma kuja nje, kuingiza vitu masikioni kunaweza kuharibu mfumo wa kujisafisha na mtu akawa anakwenda hospitalini mara kwa mara kusafishwa."

Mtaalamu huyo anasema mfumo wa sikio la nje umepinda, hivyo kuna uwezekano mkubwa mtu akajichoma na vitu anavyoviingiza sikioni na kupata maambukizo ya ngozi ya mfereji wa sikio na kusababisha uvimbe na hata kutengeneza jipu.

"Ukiweka jipu unaweza kusababisha mdomo kupooza, unakwenda pembeni. Unapooza kwa sababu neva inayopeleka nguvu kwenye misuli ya uso inapita hapo hapo kwenye mfereji.

"Unaweza kutoboa kabisa ngoma, nimekwambia ngozi ya sikio la nje inakwenda hadi kwenye ngoma. Ukitoboa ngoma halafu ngozi ikaenda sikio la kati, hii ni hatari kubwa, inatengeneza mpira ambao unakula mifupa midogo ya sikio la kati.

"Sikio la kati kwa juu limetenganishwa na ubongo kwa mfupa mwembamba wenye unene wa karatasi, ikiendelea kula mifupa inaweza kula mfupa unaotenganisha sikio la kati na ubongo wa kati.

"Kama kuna maambukizo, yanakwenda moja kwa moja kwenye ubongo. Madhara yake mtu anaweza kupata jipu kwenye ubongo au homa ya uti wa mgongo," anatahadharisha.

Dk. Mfuko pia anasema kuingiza vitu kwenye sikio kunaweza kusababisha damu kuvilia na kutengeneza bakteria ambao watasababisha maambukizo na kusambaa mwili mzima.

"Kwa sababu sikio lipo karibu na ubongo mtu anaweza kupata madhara ya kupooza, jipu kwenye ubongo au maambukizo kwenye ubongo, inaweza kuleta mpaka kifo usipoangalia.

"Ngoma ikishatoboka, haiwezi kukarabatiwa haraka kwa sababu kama kuna usaha, ni lazima utibiwe uishe. Huwezi kuweka ngoma ya bandia kukiwa na usaha, haitashika.

"Madhara ya kuweka vitu masikioni tiba yake huchukua muda mrefu mpaka miezi mitatu, ukienda hospitalini unatokwa usaha sikioni halafu ukapewa dawa ya siku tano, hapana," anasema.

Dk. Mfuko anabainisha kuwa zipo dawa ambazo wameziainisha kwa ajili ya kutumika kwa muda mrefu kwenye masikio.

"Upo mwongozo wa Wizara ya Afya kwamba daktari yeyote bingwa una leseni ya ubingwa unatakiwa ndani ya mwaka mmoja uende hospitali za vijijini kufundisha, tunajitahidi kufundisha huko ili madhara makubwa yasitokee na wagonjwa wakaletwa Muhimbili," anasema Dk. Mfuko huku akionya matumizi holela ya dawa kwa wenye matatizo ya masikio.

Anashauri watu wawe na tabia ya kuchunguza masikio yao kwa wataalamu walau mara mbili kwa mwaka, akiwa na ufafanuzi zaidi, akitamka:

"Watu waliopata majeraha kwenye kichwa, kuna mtu anakwambia sikio linatoa damu anakwenda duka la dawa anapewa matone anaweka, haturuhusu mtu kuweka majimaji yoyote kwenye sikio linalotoka damu.

"Ndani ya siku saba sikio linatoka damu, unaweka majimaji. Ukiweka hayo maji yanakwenda mpaka kwenye ubongo na kusababisha shida, ilikuwa kwenye sikio sasa inakwenda mpaka kwenye ubongo."

Dk. Mfuko anashauri sikio linapowasha ni vizuri mtu aende hospitalini kuangalia kiini cha mwasho huo badala ya kuweka ufundi kwa kuingiza vitu ndani yake.

Mtaalamu huyo anasema kupitia programu maalum wanazofanya, wamezifikia hospitali za kanda nchini na mwaka huu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usikivu Duniani, waliweka kambi Dodoma kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji wa huduma bora kwa madaktari.

Mbali na uchokonoaji wa masikio, Dk. Mfuko anataja vitu vingine ambavyo vinachangia matatizo ya usikivu kuwa ni kelele kupita kiasi na matumizi ya spika za masikioni (ear phones).

Kwa mujibu wa daktari bingwa huyo, mtu anapopata tatizo la usikivu, hupandikizwa kifaa cha usikivu kwenye sikio la ndani na huduma hiyo inatolewa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akiwa na angalizo kwamba matibabu hayo ni ghali na sasa kipaumbele nchini kiko kwa watoto wanaozaliwa wakiwa na tatizo hilo.

### HAJA YA UTAFITI

Dk. Mfuko pia anapendekeza kufanyike utafiti wa kina nchi kuhusu hali ya usikivu kwa kuwa hakuna utafiti uliofanyika nchini kuhusu suala hilo ukihusisha idadi kubwa ya watu.

Katika hilo, Nipashe Jumapili inapiga hodi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi kusaka mrejesho, naye akijibu kwamba utafiti hufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kushirikiana na taasisi zingine ziwamo MNH na vyuo vya afya.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, anaunga mkono hoja ya Dk. Mfuko ya umuhimu wa kufanyika utafiti wa kina kuhusu hali ya usikivu nchini na wanaibeba kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

Prof. Mgaya anarejea utafiti wa mwaka jana wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) na Kituo cha Udhibiti na Kinga ya Magonjwa (CDC) unaonyesha tatizo la usikivu ni kubwa duniani.

"Kwa Tanzania ili kujua ukubwa wa tatizo ninakiri bado hatujafanya utafiti huu, lakini tunaona kwa sasa unastahili kufanyika, tujue visababishi vyake na kutoa elimu.

"Tunalichukua hili tunaliweka kwenye mpango kazi wetu, tutaliandikia kwa sababu linaingia katika magonjwa yasiyoambukiza, ili utafiti ufanyike kujua hali ikoje kwa ujumla," anasema.

Kila mwaka Machi 3 ni maadhimisho ya Siku ya Usikivu. Katika ripoti yake ya mwaka 2021, WHO ilitahadharisha kuwa kufikia mwaka 2050, takribani watu bilioni 2.5 ulimwenguni watapata shida ya kupoteza kiwango fulani cha usikivu ikiwa hatua hazitochukuliwa mapema.

Idadi hiyo ni sawa na mtu mmoja katika kila watu wanne atakuwa anakabiliwa na tatizo la usikivu na kwa msingi huo, takribani watu milioni 700 watahitaji kutumia vifaa vya usikivu au tiba ya masikio na huduma nyingine za kurekebisha masikio.

# DC Gondwe ageukia madereva wazembe

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe amewataka madereva wilayani mwake kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kupunguza ajali zisizo za lazima.

Alitoa rai hiyo juzi wilayani humo wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mpango wa Usalama Barabarani Tanzania chini ya taasisi ya TARSI unaolenga kuwajenga kielimu wanafunzi walioko shuleni na wadau wengine kuhusu usalama barabarani.

Gondwe alisema serikali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi haitomvumilia mtu yeyote atakayesababisha ajali kwa makusudi, akisisitiza hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

"Mwili wa binadamu hauna spea, kwa hiyo watumiaji wa barabara pamoja na madereva zingatieni sheria. Ukiona taa nyekundu barabarani imewaka, hata kama hakuna gari, usivuke, subiri mpaka taa ya kijani itakapokuruhusu. Kwa hiyo, nipo tayari kushirikiana na taasisi hii kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa," aliahidi.

Aliwataka watumiaji wa magari katika wilaya hiyo kufunga namba za magari ambazo wamepewa na Mamlaka ya Mapato (TRA) ili iwe rahisi kutambua wahalifu wanapofanya makosa.

"Wakati ninaongea na wanafunzi, nimeambiwa kwamba wanaosababisha ajali barabarani wengi wao ni wamiliki wa magari binafsi na kuna wengine wanafunga namba za nchi za nje ili wasijulikane wakifanya kosa na wengine wanaweka namba zenye majina hata kama muda wake umeisha, hii haiko sawa," alionya.

Aliwapongeza wanafunzi waliokuwa wamekusanyika eneo ilikokuwa inatolewa elimu ya usalama barabarani, akibainisha kuwa imewabadilisha fikra na kuwaongezea uelewa juu ya masuala ya usalama barabarani.

"Ninawapongeza sana wanafunzi wa wilaya hii kwa kuwa waelewa, nimepita nimeona mmechora michoro mizuri kama zebra na mnaeleza vizuri maana ya alama hizo, hilo ni jambo zuri. Ndugu zangu wa TARSI tumekuja hapa kuwaunga mkono kwa sababu tunatambua umuhimu wa jambo hili," alisema.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Maliki Balongo kwamba wameamua kutoa elimu hiyo wakiwalenga zaidi wanafunzi baada ya kubaini wengi wao wanauelewa mdogo kuhusu sheria za barabarani

"Kama tunavyojua ajali nyingi zinasababishwa na binadamu, hivyo tumezindua programu hii ya kupita shuleni kuwapa wanafunzi elimu ya usalama barabarani, ili wajue namna ya kujiepusha na ajali na baada ya hapo tutaenda katika jamii yote," alisema.

Balongo alisema taasisi hiyo haitaishia Dar es Salaam pekee, bali itaifikia mikoa mingine ya Tanzania ili kutanua wigo katika kufikisha elimu hiyo.

# 33,000 wafariki kila mwezi kutokana na moshi wa kuni

**Na Renatha Msungu ,**
DODOMA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amesema moshi wa kuni za kupikia unaua watu 33,000 kwa mwezi kutokana na kutengeneza sumu inayoua taratibu huku ukichangia kuharibika kwa mimba.

January alitoa kauli hiyo juzi alipofungua semina kwa wabunge wanawake kuhusu masuala ya nishati ya kupikia iliyofanyika jijini hapa.

Alisema, wanawake wengi wa vijijini na mijini wamekuwa wakiathirika kutokana na moshi wa kuni ambazo hutumika kupikia katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuuvuta wakati wanapika.

"Kila siku iendayo kwa Mungu wanawake wa mjini na vijijini wanameza moshi unaoathiri afya zao, hivyo kama wizara tunahitaji kutatua hili ili kuokoa maisha ya kinamama ambao ndiyo wanaopika," alisema.

Waziri huyo alisema athari nyingine kubwa kwa wanawake kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, ni mimba kuharibika na watoto kuzaliwa kabla ya muda.

Alisema, unyanyasaji wa kijinsia upo kwa wingi kwa wanawake hususani wa vijijini pale wanapotumia nishati ya kuni, akifafanua kuwa kipindi cha mvua nishati hiyo imekuwa ikileta shida na kusababisha chakula kuchelewa na kuambulia kipigo kutoka kwa waume zao.

"Wanaume wengi wamekuwa wakiwapiga wanawake pale wanapokuta chakula hakijawa tayari, haijalishi kuna mvua ambayo inachangia kuni kuchelewa kuwaka," alifafanua.

Kutokana na hilo, Waziri January aliwataka wabunge wanawake na viongozi wengine kulisemea suala hilo wanapokwenda kwa wananchi kwa kuwa wanaoathirika hawana sauti ya kulizungumzia.

"Ninaomba hili suala liwe kama ishu ya mafuta inavyopigiwa kelele na hili lipigiwe kelele ili kuokoa maisha ya wanawake," Waziri January alisisitiza.

Alisema, wao kama wizara wanaweka mikakati ya kuhakikisha wanakabiliana nalo ili kuokoa maisha ya watanzania wanaotumia nishati ya kuni na badala yake watumie nishati ya gesi. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usambazaji Umeme Vijijini (REA), Hassan Said alisema wataendelea kusambaza nishati vijijini ili kuhakikisha jamii inabadilika na kuanza kutumia nishati ya gesi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake (TWPG), Shally Raymond, aliishukuru Wizara ya Nishati kwa kutambua umuhimu wa suala hilo huku akiwataka kulipigia kampeni suala hilo ili lifanyiwe kazi.



Mkufunzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Tausi Msangi (kulia), akitoa mafunzo ya jinsi ya kutengeneza mkaa mbadala kwa akinamama viongozi wa Kanisa la Moravian Usharika wa Segerea, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARURA yaja na mkakati kupunguza gharama ujenzi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIKA kukabiliana na gharama kubwa za ujenzi wa barabara na madaraja, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), umeanza mkakati wa kutumia teknolojia ya mawe ambayo inaokoa gharama kwa asilimia 50.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seif alibainisha hayo juzi jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu teknolojia hiyo wakati wa maazimisho ya Siku ya Wahandisi yaliyoambatana na maonyesho ya kazi mbalimbali za kihandisi.

Seif, alisema TARURA imeanza mkakati wa kutumia teknolojia ya ujenzi wa madaraja na barabara kwa kutumia mawe badala ya nondo na zege ili kupunguza gharama za ujenzi.

"Teknolojia ni mojawapo ya mkakati wetu wa TARURA, kujenga madaraja na barabara na kutumia vifaa ambavyo viko katika eneo ambalo ujenzi huo unafanyika," alisema.

Seif alisema, manufaa ya teknolojia hiyo ni bei kuwa chini kwa kuwa vifaa vyote vinapatikana katika maeneo ya mradi.

Aliongeza kuwa wameshajenga kwa mawe katika madaraja zaidi ya 72 mkoani Kigoma kwa Sh. milioni 1.4 na kwamba ujenzi huo unaendelea kwenye mikoa ya Mwanza, Iringa na Singida.

Alisema ujenzi huo ni nafuu kwa kuwa vifaa vinapatikana katika eneo la ujenzi na kwamba mkakati wao ni kuangalia maeneo yote yenye mawe.

Alisema, kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji wanatoa mafunzo mkoani Kigoma kwa mafundi kutoka maeneo mengine ya Kilimanjaro, Iringa na Singida.

"Gharama za ujenzi zinapungua kwa zaidi ya asilimia 50, ukitumia zege na nondo utakuta ni gharama zaidi ya mara mbili. Teknolojia hii inatumia saruji, mchanga na mawe,"alisema.

Mtendaji huyo alisema mawe yanayotumika katika ujenzi wa barabara yanatakiwa yawe na ubora na yachongwe na kupangwa vizuri kwa ajili ya ujenzi.

Mmoja wa wahandisi kutoka TARURA, Phares Ngeleja alisema wana mpango wa kuendesha mafunzo kwa wahandisi ili waifahamu teknolojia hiyo kwa kuwa wao ndiyo watakuwa wanaisimamia katika maeneo yao.

"Kuanzia mwezi Februari, tutakuwa na mafunzo yatakayofanywa na wenzetu Wabelgiji, tutaanzia mikoa kadhaa na baadaye tutasambaa nchi nzima," alisema Ngeleja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ulinzi taarifa binafsi itadhibiti uvujishaji wa siri

**BUNGE** la Tanzania juzi lilimaliza mkutano wake wa nane jijini Dodoma huku mambo mbalimbali yakijadiliwa na kupitishwa ikiwamo serikali kusikia kilio cha wananchi kuhusu tozo za miamala ya kielektroniki kwa maana ya simu za mkononi na benki.

Pamoja na suala hilo la tozo, Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa mwaka 2022 ulisomwa kwa mara ya kwanza na unatarajiwa katika mkutano ujao, utakaofanyika Novemba, utajadiliwa na kupitishwa kabla ya kutiwa saini na Rais na kuwa sheria. Muswada huo pamoja na mambo mengine, unaonyesha kuwa ni mkombozi kwa watu wengi kutokana na kilio cha muda mrefu kuhusu taarifa za watu kudukuliwa kupitia kampuni na taasisi au watu binafsi. Watu wamekuwa walilalamika kudukuliwa kwa taarifa zao au kuvujishwa na matokeo yake kupata matatizo makubwa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Katika muswada huo, kuna adhabu kali zitakazotolewa dhidi ya wahusika watakaovujisha au kutoa taarifa za watu bila ridhaa yao. Kampuni au shirika linalofanya makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi, ikiwamo kuuza taarifa, imependekezwa kutungwa sheria itakayokuwa na adhabu ya faini isiyopungua Sh. milioni moja na isiyozidi Sh. bilioni tano.

Aidha, ikiwa ni mtu binafsi atakayebainika kutenda kosa na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 60 (6) (a) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022, atalipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 20 au kifungo kisichozidi miaka 10 au vyote kwa pamoja.


Kuhusu makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi, sheria hiyo inapendekeza atakayetiwa hatiani kwa kutenda makosa hayo, kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Adhabu ya jumla chini ya kifungu cha 63 (b) cha sheria hiyo inaelekezwa kuwa baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya sheria hiyo, mahakama inaweza kuamuru kukamatwa kwa vifaa vyake vyenye taarifa binafsi vilivyohusika katika kutenda kosa. Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo inaeleza kuwa mkusanyaji ambaye bila sababu za msingi, atafichua taarifa binafsi kwa njia yeyote ambayo haiendani na madhumuni ambayo taarifa hiyo imekusanywa, atakuwa anatenda kosa.

Kwa mantiki hiyo, iwapo mtu atapata taarifa binafsi au atapata taarifa yoyote inayojumuisha taarifa binafsi bila idhini ya mkusanyaji au mchakataji, ambaye anahifadhi taarifa hiyo, atafichua taarifa binafsi kwa mtu mwingine atakuwa ametenda kosa. Pia mtu atakayeuza taarifa binafsi, ambayo imepatikana kwa ukiukwaji wa sheria inayokusudiwa kutungwa, atakuwa ametenda kosa. Kutokana na kuwasilishwa kwa muswada huo, serikali inastahili pongezi kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba taarifa za watu, wakiwamo viongozi na watu mashuhuri, kwamba taarifa zao zikiwamo za siri zinavujishwa, hivyo kupata madhara kwa namna mbalimbali. Mmoja wa viongozi waandamizi na walioitumikia serikali kwa muda mrefu katika nyadhifa mbalimbali na kwa uaminifu, aliwahi kulalamika taarifa zake kudukuliwa na kutolewa hadharani. Hatua hiyo ilisababisha kufungua shauri mahakamani ambalo lilimpa ushindi na mtu aliyemchafua kutakiwa kumlipa mabilioni ya shilingi.

Mbali na kiongozi huyo, wako pia viongozi wastaafu wa serikali na taasisi za umma waliwahi kuchafuliwa kupitia mitandao ya kijamii na matokeo yake kupata athari za kisaikolojia na kiafya. Kwa ujumla, muswada huo, pindi utakapopitishwa na hatimaye kuwa sheria, kwa kiasi kikubwa utasaidia kukomesha na kudhibiti tabia za baadhi ya watu waliokuwa na tabia ya kuingilia mambo ya watu, yakiwamo yale ya ndani, na kusambaza. Kutungwa sheria ni jambo moja lakini utekelezaji ni kitu kingine. Ni muhimu kwa vyombo vilivyopewa dhamana ya utekelezaji wa sheria, pindi sheria hiyo itakapopitishwa na kutiwa saini kwa ajili ya kutumika, vikasimamia kwa ukamilifu ikiwamo kufanya uchunguzi na kuhakikisha wahusika wanafikishwa katika vyombo vya utendaji haki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Chakula shuleni suluhisho la utoro

**WANAFUNZI** wa shule za msingi na sekondari nchini, wamekuwa wakikumbana na kikwazo cha kutofanya vizuri katika masomo, kutokana na sababu mbalimbali, mojawapo ikitajwa kuwa ukosefu wa chakula shuleni.

Ukosefu huo wa chakula, unaelezwa kuwa unasababisha wanafunzi kukosa usikivu darasani au kuwa watoro na hata wakati mwingine kuacha shule, hali ambayo inaweza kukwamisha malengo yao kwenye elimu.

Ziko pia sababu mbalimbali zinazochangia shule kukosa chakula, ikiwamo baadhi ya wadau wa elimu kama wazazi na walezi kutojua au kutokuwa tayari kuchangia chakula cha shule kwa ajili ya watoto wao.

Ninadhani kuna haja kwa wazazi na walezi kutambua kuwa wao ni wadau muhimu wa elimu, hivyo ingependeza kama watakuwa tayari kuchangia chakula shuleni, kwa ajili ya watoto wao.

Wako baadhi yao ambao huwa hawako tayari kusikia suala la kuchangia chakula au fedha kwa ajili ya watoto wao, huku wakidai kwamba serikali ilishatangaza kutoa elimu bure na pia imezuia kuwapo kwa michango shuleni.

Baadhi ya walimu wamekuwa wakiripotiwa kwenye vyombo vya habari wakilalamika hali hiyo ya wazazi kutochangia fedha, kwa ajili ya chakula cha mchana kwa watoto wao na kusababisha wawe watoro shuleni.

Kwa ujumla ni kwamba, suala la uwapo wa lishe shuleni linaweza kusaidia kupanua wigo wa usikivu kwa wanafunzi, kwa sababu wanakuwa wamepata chakula na kuchochea wingi wa mahudhurio.

Umuhimu wa chakula shuleni, unaifanya serikali iwatake wadau wa lishe kushiriki na kusaidia mpango wa lishe shuleni, ili kusaidia kupunguza utoro na kuongeza mahudhurio na umakini wa wanafunzi darasani.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alibainisha hayo wiki iliyopita kwenye hafla ya kutia saini fomu ya muungano wa lishe shuleni iliyotengenezwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

Anasisitiza kuwa mradi huo ni muhimu kwa shule, kwa kuwa unasaidia kuchochea mahudhurio ya wanafunzi, usikivu wa darasani lakini pia kuwajengea afya bora wanafunzi wanaohudhuria shuleni.

Wakati serikali ikiwa na mikakati ya uhamasishaji wa chakula shuleni, wazazi na walezi nao wangekuwa na mwamko wa kuchangia chakula, ili kuyafanya mazingira ya shuleni kuwa rafiki kwa watoto wao.

Kimsingi ni kwamba, bila wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla kusaidia upatikanaji wa chakula cha mchana kwa wanafunzi shuleni, lengo la serikali la kuhakikisha inaboresha elimu kwa kila mtoto linaweza lisifikiwe.

Badala yake, kunaweza kuibuka matabaka kwa baadhi ya wanafunzi, wakiwamo wanaopata chakula cha mchana na wengine kukosa kabisa, hivyo wadau hao wa elimu hawana budi kuchangia maendeleo ya watoto wao.

Sidhani kwamba ushindani unaweza kuwa sawa kwa kila mmoja, wakati elimu inatolewa bure ni muhimu pia watoto wote wapate chakula cha mchana shuleni, kwani si vyema kuona baadhi wakipiga miayo, huku wengine wakila.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inakiri kuwa kupata matokeo mazuri ya elimu ni muhimu kuwapo lishe bora shuleni, ili kuwajengea wanafunzi afya bora na kuwa na utulivu wa akili wawapo madarasani.

Kwa umuhimu huo wa chakula shuleni, ninadhani ni wakati sahihi sasa jamii na Watanzania kwa ujumla kushiriki kikamilifu kwenye suala la upatikanaji wa chakula shuleni ili kuboresha elimu na afya za watoto.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Ijue Mahakama ya EAC isiyo na rufani na hukumu zinavyopuuzwa



Na Pascal Mayalla

SAFU hii ya 'Kwa Maslahi ya Taifa', inaendelea na makala elimishi za kuijua Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambako mwanasheria wako Wakili Pascal Mayalla, anakuzamisha kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki sura kwa sura. Leo tunaanzia Sura ya nne ambayo inazungumzia Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sura hii inajumuisha Ibara ya 23 mpaka Ibara ya 47 kuhusu Mahakama ya Afrika Mashariki. Chanzo chake ni makubaliano ya nchi wanachama kuainisha na kuoanisha mifumo ya sheria ya nchi zao ifanane ili wakati mtangamano utakapokamilika, hii ndiyo itakuwa mahakama ya juu ya Afrika Mashariki.

Kwa kuanzia, mahakama hii imepewa uwezo wa kupokea na kusikiliza mashauri yatokanayo na migongano katika Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki tu. Mahakama hii pia inapokea mashauri ya masuala ya haki za binadamu.

Hata hivyo, kuwepo kwa Mahakama hii hakutaondoa uwezo wa mahakama za kitaifa katika nchi wanachama lakini itatumika kama sehemu ya rufani isipokuwa pale inapotajwa waziwazi kuwa jambo fulani litakuwa chini ya mahakama hiyo tu. Mahakama hii ndiyo pekee yenye haki zaidi ya kutafsiri Mkataba wa Afrika Mashariki kuliko mahakama za kitaifa.

Kwa bahati mbaya ule ukoloni mamboleo wa kutumia lugha za wakoloni pia umebebwa na mahakama hii. Mahakama ya Afrika Mashariki itatumia lugha ya Kiingereza. Ningefanikiwa kuingia kwenye Bunge la Afrika Mashariki (EALA), hili la matumizi ya lugha adhimu ya Kiswahili ingekuwa ajenda yangu kuu ya kuipigania. Wakati Jumuiya ilipoanzishwa na nchi tatu - Tanzania, Kenya na Uganda, kwa vile zote pia zinatumia Kiingereza kama lugha, hili la kutumia Kiingereza lilikuwa sawa lakini sasa jumuiya imetanuka, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zenyewe zinatumia Kifaransa na Kiswahili. Hazitumii Kiingereza, hivyo Tanzania lazima tujifunze kuweka baadhi ya agenda na kuzipigania. Kukipigania Kiswahili kiwe lugha rasmi ya Mahakama hii ni jambo la maana sana.

Mahakama hii makao yake makuu yako Arusha, Tanzania. Ibara ya 24 inahusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama. Inaelezwa kuwa majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki watateuliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Kimsingi, wanapaswa kutoka katika nchi wanachama wa Jumuiya, yaani Kenya, Tanzania na Uganda.

Majaji hawa wanapaswa kuwa waadilifu na kutopendelea upande wowote na hapa sasa ndipo umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili unapozidi, huwezi kupata Jaji kutoka Rwanda, Burudi na DRC anayezungumza Kiingereza, ila Kiswahili wanazungumza.

Nchi zilipokuwa tatu, idadi ya majaji ilikuwa sita kwa kila nchi mwanachama kuteua majaji wawili. Mahakama itaongazwa na Rais wa Mahakama na Makamu Rais wa Mahakama. Urais huu utakuwa wa mzunguko kati ya nchi wanachama.

Ibara ya 28 mpaka 30 zinahusu malalamiko kwenye Mahakama. Mtu yeyote kutoka nchi wanachama anaweza akapeleka malalamiko yake katika mahakama hii. Hata hivyo, malalamiko haya ni yale tu yenye nia ya kuhoji uhalali wa kanuni, agizo, uamuzi au kitendo chochote cha nchi mwanachama au chombo chochote cha Jumuiya ni kutaka kuonyesha kuwa kitendo kilichofanyika ni kinyume cha vifungu vya mkataba wa ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Malalamiko mengine yatakayoweza kupelekwa kwenye Mahakama hii ni yale yanayohusu migogoro kati ya wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya yenyewe.

Ibara ya 31 hadi ya 37 zinahusu mashitaka. Mashitaka yanaweza kupelekwa katika Mahakama hiyo kwa maandishi au kwa mdomo. Walalamikaji katika Mahakama hiyo wanaweza kusimama wenyewe mahakamani au wakawakilishwa na mawakili au washauri wa kisheria. Mshauri huyo wa kisheria atakuwa na haki ya kufika mahakamani kila wakati shauri linapotajwa au kusikilizwa. Ibara ya 38 mpaka 40 zinahusu hukumu na kwamba moja ya hatua za kwanza ambazo Mahakama inaweza kuchukua katika uwezo wake wa hukumu ni kutoa amri za muda. Amri za muda au maagizo yoyote vinatumika kuzuia jambo fulani kuendelea kufanyika hadi Mahakama itakapotoa amuzi wa mwisho. Pia nchi wanachama zinaagizwa kuwa mara mashauri yapelekwapo katika mahakama hiyo, nchi wanachama zitaacha kushiriki katika kitendo chochote kile ambacho kinaweza kuharibu usuluhishi wa ubishani huo, au hata kuukuza zaidi.

Katika kutoa hukumu, Mahakama inaweza kutoa uamuzi au maamuzi ya awali ambayo hutangulia hukumu. Maamuzi ya awali sio hukumu kwa maana halisi ya hukumu, bali ni hatua ya Mahakama kueleza msimamo wake juu ya kipengele fulani ambacho kinabishaniwa, na ambacho ni sehemu ya kesi nzima.

Baada ya kutolea uaamuzi vipengele vyote vinavyobishaniwa na baada ya kupokea hoja za pande zote mbili, Mahakama itatoa hukumu yake. Hukumu hii itakuwa ndiyo msimamo uliofikiwa na majaji wengi. Baada ya hukumu kutolewa, nchi mwanachama au wanachama au vyombo husika vitakuwa na jukumu la kutekeleza maagizo ya hukumu hiyo.

Katika utekelezaji wa hukumu za mahakama hii, kuna tatizo la kisheria na kimfumo, hakuna takwa lolote la kisheria hukumu za mahakama hii kusajiliwa na mahakama husika, ili zisipotekelezwa zitolewe amri za kukazia hukumu hizi, matokeo yake ni nyingi ya hukumu za mahakama hii hupuuzwa na nchi husika! Nikiwa mwanasheria, kule EALA ningesaidia kufanya marekebisho hukumu za mahakama hii zisajiliwe na mahakama za nchi husika ili zitekelezwe.

**Mahakama Haina Rufani**

Mahakama ya Afrika Mashariki haina utaratibu wa kukata rufani kwenda mahakama nyingine yoyote, Hata hivyo, upande ambao haujaridhishwa na uamuzi uliotolewa unaweza kutoa maombi ili mahakama ifanye mapitio ya uamuzi wake wa awali.

**Wiki Ijayo tutaliangazia Bunge la Afrika Mashariki. Tukutane panapo majaliwa.**

**Wasalaam Paskali**

**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ukitaka kujifunza siasa chungulia ndani ya CCM



Na Joseph Kulangwa

KUNA vuguvugu la kisiasa linaendelea nchini lakini kwa chinichini na kwa ustadi mkubwa, watu wakiogopa kukanyaga nyaya, shoo ikakatika. Hiyo inazingatia kubakiwa na miaka miwili tu ya kufikia uchaguzi mkuu.

Ndani ya Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), mambo yanaonekana kupikwa kwa nguvu huku kuni zikichochea moto kwa bidii kubwa, watu wakiangalia ifikapo mwaka 2025 nani atakuwa nani na kama atasimama mmoja au wengi kujitokeza.

CCM ndicho chama kiongozi kwa sasa ambacho wengi wanakitazama na kukiangalia kitakuja na utaratibu gani ifikapo mwaka huo na ndipo vyama vingine vitatia mguu na kujipima mbavu kuona kama vitakiweza.

Msimamo wa chama hicho tawala mpaka sasa angalau ni kumsimamisha Rais Samia Suluhu Hassan kupeperusha bendera yake mwaka huo, kikiamini kwamba kitakuwa kipindi chake cha pili cha kumalizia ifikapo mwaka 2030.

Lakini ndani na nje ya chama hicho, kuna wasiokubali msimamo huo, wakisema hastahili kugombea mwaka 2025 kwani atakuwa ameshamaliza kipindi cha pili cha awamu yake wakati wanaomwunga mkono wanasema ni awamu ya sita, huku wa upande wa pili wakishikilia kuwa ni ya tano.

Iko hivi, baada ya Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere kung'atuka mwaka 1985 alishakaa Ikulu kwa takriban miaka 24, sawa na awamu mbili na ushei za sasa. Alipomwachia Rais wa Pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ndipo utaratibu usio kwenye Katiba ukaanza wa vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Hiyo ilimaanisha kwamba Rais akishachaguliwa kutoka chama hicho, alipewa fursa ya kugombea tena miaka mingine mitano ili kukamilisha awamu yake ya uongozi. Ndivyo ilikuwa kwa Rais wa tatu, Hayati Benjamin Mkapa, ikawa hivyo kwa wa nne, Jakaya Kikwete. Ilitakiwa kuwa hivyo kwa Rais wa tano, Dk. John Magufuli, lakini Mungu hakupenda iwe hivyo na kwa kudra zake, akamchukua akiwa amebakiza takriban miaka minne amalize vipindi vyake viwili kama ilivyo ada ya CCM.

Baada ya kifo chake, aliyekuwa Makamu wake, Samia, akaapishwa kuwa Rais. Lakini wakati watu wakiamini kwamba ni Rais wa awamu ile ile ya tano kwa kuwa alikuwa anamalizia kipindi chao na Magufuli, ikatangazwa kuwa ni wa awamu ya sita.

Waliokuwa wanaamini kuwa bado ni awamu ya tano, wakasema ni Rais wa sita katika awamu ya tano, kwa kuzingatia utaratibu waliojiwekea wa miaka mitano mitano kuwa awamu moja.

Waliodhani wanajua zaidi, wakafafanua kwamba mtu anapokuwa mgombea mwenza katika kinyang'anyiro cha urais, anakuwa sehemu ya awamu husika, hivyo Rais akifariki dunia, yeye atamalizia kipindi kilichosalia na si kuanza upya.

Wakasema ingewezekana hata cheo cha Makamu wa Rais kingeitwa Rais Mwenza kama ambavyo kuna Mwenyekiti Mwenza katika taasisi na kampuni mbalimbali kwa maana wote wanaongoza nchi kwa sera, msimamo, mfumo na imani moja, hivyo hapana sababu ya kuwatenganisha.

Kwa dhana hiyo, ina maana Rais Samia anaongoza nchi kwenye viatu vya Magufuli kwa sababu walichaguliwa kwa karatasi moja ya kura, hivyo ushindi wa Magufuli ulikuwa ushindi pia wa Samia.

Walifika mbali na kusema hata kuapishwa kwa Samia hakukuwa na ulazima, kwa sababu kiapo cha Magufuli kingeweza kutosha ila tu, pengine kutokana na kila mtu kuwa na imani na fikra zake, ndipo hulazimika kuapa kila mmoja kivyake.

Wenye kufikiri hivyo ndio wanaosema kuwa labda kwa sababu zingine, Rais Samia anapaswa kumalizia kipindi cha awamu ya tano mwaka 2025 na kupisha agombee mwana CCM mwingine. Hilo ndilo linalofikirisha watu hususan waliomo CCM na hasa wanaochochea kuni za kutaka kugombea urais kipindi kitakapojiri.

Inawezekana kuweka mgombea mwenza wa urais, kulikuwa na nia njema ya kusaidia kama yatatokea majanga kama yaliyotokea kwa Dk Magufuli, mara moja bila kutumia gharama kubwa za kurudi kwenye uchaguzi, apishwe Makamu kuchukua hatamu za uongozi na kazi iendelee. Hata hivyo, hakuna mwenye mamlaka ya kuiamulia CCM nini cha kufanya bali yenyewe itaona linalofaa katika hilo na kumsimamisha Samia au kumleta mwingine kwa jinsi watakavyokubaliana wao kwenye vikao vyao vya ndani.

Bila shaka, ana nafasi kubwa kutokana na muktadha uliopo, ikiwa ni pamoja na alichokifanya mpaka sasa tangu achukue madaraka ya urais, na hicho ndicho kitakachoamua kwa wanaowania urais ama kusuka au kunyoa. Katiba zitahusika kwa hili. Alamsiki!

**kulangwasos@gmail.com**

# Waonywa kuyagawa mashamba yaliyofutwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro amewaonya maofisa ardhi wa wilaya zote wa mkoa huo kugawa kwa wawekezaji wengine ardhi ya mashamba pori 11 yaliyofutwa na Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni.

Fatma Mwasa, alitoa onyo hilo jana baada ya kupewa nafasi ya kuwasilisha salam za serikali katika kikao maalum cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani hapa.

Alisema, wapo baadhi ya wataalamu wa ardhi waligawa mashamba pori yaliyofutwa na serikali ya awamu iliyopita wakati maagizo yalielekeza kuwapa wakulima na wafugaji wa maeneo husika ili kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi.

Alisema, kwenye utendaji kazi amejielekeza katika maeneo makubwa matano yakiwamo ya huduma za jamii ambako atatumia muda mwingi, nguvu na maarifa na wataalamu wa kutosha ili kutatua shida mbalimbali za wananchi, ukiwamo utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Mkoa alisema, Rais alishafuta mashamba pori 11 yaliyopo katika baadhi ya halmashauri za wilaya za mkoa huo, lakini katika 'pitapita', amebaini wataalamu wa ardhi wameshakuwa na mipango mingine ya wawekezaji.

"Ninawaonya wataalamu wa ardhi kwamba ardhi iliyofutwa na Rais Samia Suluhu Hassan, itakwenda kwa wakulima wanyonge, wadogo na si kwa wawekezaji kwani wawekezaji wa sasa ni wananchi wenyewe," alisema. Mwasa alisema, yapo maeneo mengine yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji ambako hakutakuwa na shughuli za kilimo, hivyo kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Ipo migogoro ya ardhi lakini hatujakaa chini kuijadili, hivyo ninawaomba wabunge wa mkoa wetu, wenyeviti wa halmashauri na viongozi wa chama tukae pamoja ili tupate maelezo kwa nini migogoro ni mingi Morogoro?' Mwasa aliagiza.

Alisema, viongozi waliotangulia waliekeza nguvu nyingi na kutoa maeneo makubwa ya ardhi kwa watu walioitwa wawekezaji ambao hadi sasa wanayaendeleza na matokeo yake wananchi hawana ardhi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali.

"Kutokana na wananchi wengi wao kukosa ardhi imepelekea kuwapo uvamizi ndani ya mkoa wetu, sasa lazima tuwarudishie ardhi yao na ninaposema ninawaomba ushirikano wa dhati ili kumaliza shida hizi," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro, Dorothy Mwamsiku aliishukuru serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa mkoa huo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi.



Mkurugenzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladislaus Mwamanga (wa tatu kulia), akionyesha bwawa la maji lililochimbwa na walengwa kwa mpango wa kuhudumia kaya maskini katika Kijiji cha Ikombolinga, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. Kulia ni Mwenyekiti wa mtandao wa wabunge wa Benki ya Dunia na Mbunge wa Jimbo la Birmingham Uingereza, Liam Byrine na (wa pili kulia) ni Mwenyekiti wa mtandao huo nchini na Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Miundombinu kuboreshwa kuvutia wawekezaji nchini

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema itaendelea kuimarisha miundombinu nchini ili kuwavutia zaidi wawekezaji watakaosaidia taifa kupunguza kuagiza bidhaa nyingi kutoka nje ya nchi.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaude Kighae, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya 23 ya Afrika Mashariki ya Teknolojia na Uhandisi jijini Dar es Salaam.

Maonyesho hayo yameandaliwa na Kampuni ya Teknolojia kutoka China ya EEPCINDIA, kwa kushirikiana na Ubalozi wa ya India nchini na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo ya Tanzania (TCCIA).

Kighae alisema, maonyesho hayo yatatoa fursa kwa wawekezaji wa nje kuziona fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania.

"Kwa kupata fursa kama hizi za kuwaleta pamoja wafanyabiashara mbalimbali, kunatoa nafasi ya kupata wawekezaji wapya. Kwa kulitambua hili, serikali tunaendelea kujenga mazingira mazuri na rafiki kwa wawekezaji, tutaendelea kuboresha miundombinu kama barabara, reli na bandari zetu," alisema Kighae.

Alibainisha kuwa zipo fursa nyingi za uwekezaji nchini hasa katika kilimo na viwanda.

Mkurugenzi wa Ukanda wa Uwekezaji wa Kiuchumi (EPZA), Charles Itembe, alisema Tanzania ina maeneo maalum ya uwekezaji ambayo wawekezaji wanaweza kuwekeza.

"EPZA tupo kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji kufanya biashara zao kwa uhuru, tunawasaidia kupata vibali vya kuwekeza, niweke wazi yapo maeneo ya uwekezaji kama Nyanda za Juu Kusini, eneo la maziwa pamoja na maeneo ya Pwani, huko kote tunakaribisha wawekezaji," alisema Itembe.

Aliishukuru Serikali ya India, kupitia ubalozi wake nchini kwa kuichagua Tanzania kama kituo cha cha kufanya maonyesho hayo.

Balozi wa India nchini, Binayak Srikanta Pradhan, alisema Tanzania imekuwa na ushirikiano mzuri wa kihistoria na India na ndiyo sababu ya kufanyika kwa maonyesho hayo.

Alisema Tanzania imekuwa kitovu cha uagizaji vifaa na mashine za uhandisi kutoka India kuja Afrika Mashariki.

"Ni maonyesho ambayo yataendelea kutoa fursa za Uwekezaji kwa pande zote, Tanzania imekuwa mshirika mkubwa wa India katika kusafirisha bidhaa mbalimbali kuja Afrika Mashariki," alisema Balozi Pradhan.

Mwenyekiti EEPCINDIA, Mahesh Desai alisema India ni moja ya wasambazaji wakubwa watano wa vifaa vya uhandisi vinavyoingizwa Tanzania na Afrika Mashariki.

"Maonyesho haya ni hatua mojawapo ya ushirikiano wenye faida kwa nchi zote za Tanzania na India," alisema Desai na kubainisha kuwa wamekuja wafanyabiashara mbalimbali kwenye sekta ya teknolojia ya uhandisi kuangalia fursa zilizopo Tanzania.

## Wasifu utekelezaji mpango wa TASAF

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MWENYEKITI wa Mtandao wa Wabunge wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa, Liam Byrne ameeleza kufurahishwa na utekeleza wa mpango wa kuhudumia kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Byme, ambaye pia ni Mbunge wa Birmingham, Uingereza na Waziri wa Fedha wa zamani, alibainisha hayo jana kwenye ziara ya kutembelea walengwa wa TASAF katika Kijiji cha Ikombolinga wilayani Chamwino mkoani Dodoma.

Alisema, amefurahishwa kuona ushirikiano unaofanywa katika utekelezaji wa mradi huo wa TASAF, jambo linalowanufaisha walengwa wa mpango huo.

"Nimefurahishwa sana na utekelezaji wa mpango huu na walengwa wa TASAF wananufaika, ninawapongeza wasimamizi wa mpango huu ambao ni TASAF kwa kazi kubwa wanayofanya," alisifu Byrne.

Alisema, mafanikio hayo yanaonyesha jinsi TASAF wanavyothamini mchango wa fedha unaotolewa kwa ajili ya kuzisaidia kaya maskini na kuongeza kuwa kinachofanyika kinapaswa kutambulika duniani ili wengine waige mfano.

"Niondokapo Tanzania lazima nikasimulie mafanikio haya, nimefarijika sana kuona walengwa wa mpango huu wana sura zenye bashasha," alisema Byrne.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Wabunge wanaosimamia fedha za Benki ya Dunia (WB) nchini na Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangila, alisema wamefarijika kuona fedha zinazotolewa na benki hiyo zinafanya kazi stahiki kwa walengwa wa mpango huo.

Alisema, wao kama wabunge watakuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ili zifike sehemu sahihi na kwa wakati.

Mkurugenzi wa TASAF, Ladislaus Mwamanga alisema mpaka sasa tayari wametekeleza miradi mingi katika awamu hii ya kwanza, hivyo wanaendelea ili kuwafikia walengwa wote waliopo ndani ya mpango huo.

Alisema mradi wa uchimbaji mabwawa umesaidia kutoa ajira kwa walengwa wa mpango huo ikiwamo kujipatia kipato kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Mlengwa wa mpango huo, Magreth Puma aliishukuru serikali kuwaletea mpango huo ambao umemwezesha kujenga nyumba na kusomesha wanawe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dk. Semutatus Mashimba, alibainisha kuwa jumla ya walengwa 437 wako katika halmashauri hiyo na mpaka sasa wametumia Sh. milion 190 zinazotolewa kwa ajili ya walengwa wa mpango huo.

MAISHA
SEPTEMBA 25, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14


## Vyakula vinavyopunguza mwili

## MAISHA NI NYUMBA

MSIMU wa kupanga nyumba sasa unakaribia, usikurupuke



Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# MIILI ILIYOJENGEKA

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | J | U | M | B | A |
| ■ | A | ■ | ■ | O | ■ |
| U | M | O | ■ | M | ■ |
| ■ | B | ■ | P | A | A |
| ■ | I | ■ | ■ | N | ■ |
| K | A | M | B | I | ■ |

## AMSHA AKILI


TUMIA RANGI YA NJANO NA NYEKUNDU TU, KUMREJESHEA RANGI KIPEPEO HUYU



## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IBA, ONA, YANGA, DIMBA, BAMBIA, DONYOA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akizungumza na rafiki yake wakitoka shuleni.

Juma: Hivi leo umemuelewa mwalimu wa bailojia?

John:Nimemuelewa sana tu

Juma: Hivi itakuaji wale vikambale vidogo vikageuka kuwa vyura?

John: Wale sio samaki kambale wadogo bali ni hatua ya ukuaji wa chura, anaanza kama yai, wanakuja kuwa viluilui na kisha anakuwa chura kamili.

**SWALI**

**Mbu analeta athari zipi kwa binadamu?**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Laana itakupiga ukidharau wazazi kwa kufanikiwa

KARIBU tena msomaji wangu tuifunde jamii yetu, hasa vijana wanaoinukia kimaisha. Kumbuka kwa wale wanaofuatilia safu hii, wiki iliyopita nilieleza sana umuhimu wa wazazi katika malezi ya familia.

Wazazi ni walezi wakuu kwa neema waliyopewa na Mungu, hivyo wanastahili heshima na ushauri wao ni dira ya maisha yetu. Wako vijana wengi wamesomeshwa na kupata kazi nzuri, nafasi za juu serikalini lakini wanajiinua na kuanza kuwadharau wazazi.

Wanasahau kwamba hawa ndio waliojifunga mkanda na kujinyima ili wasome na kufikia hapo walipo. Lakini wanawasahau au kuwadharau kana kwamba hawahusiki na lolote kuhusu mafanikio yao!

Lakini ukweli ni kwamba hata ukifanikiwa kwa kiwango gani, ni hatari sana kuwasahau wazazi wako au walezi wako. Si vibaya kuwathamini walezi wako wa hiari.

Lakini si vyema kuwasahau wazazi wako wa kukuzaa kwa sababu tu ya nafasi yako kazini au elimu yako uliyowazidi wazazi wako walioishia darasa la saba, au la nne kisa eti wewe umesoma, una digrii za kutosha. Je, msingi wa kufika hapo si juhudi za wazazi wako?

Yaani unawaweka pembeni na kuwakumbatia wazazi wa hiari eti kwa hadhi yako unahitaji kuwa na mama wa aina hii au baba wa aina hii. Hapana! Hiyo ni kwenda tofauti na neno la Mungu kwani unaingia kwenye kuwadharau wazazi wako!

Mungu katika neno lake (Kumb. 27:16) anasema, “Na alaaniwe amdharauye baba yake au mama yake. Na watu wote waseme Amina”. Watu wengi hii leo wanatembea na laana kwa kuwadharau wazazi wao. Wengine hudhani wamelogwa kumbe ni laana ipo juu yao.

Yaani wewe unamdharau mzazi wako kwa jinsi ulivyo? Eti umeshafika mjini, umepata marafiki wazuri, wenye majina makubwa.

Kwa hiyo unaona kule kijijini siyo kwako tena, wale uliowaacha wakiwamo wazazi hawakuhusu tena!

Huenda ni miaka 10 hadi 15 hujarudi tena huko, kwani eti hakuendani na wewe. Hujafuatilia hata wazazi wako wanaendeleaje, hiyo ni kuwadharau. Neno la Mungu linasema, “Waheshimu baba yako na mama yako, kama BWANA, Mungu wako alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi akupayo BWANA, Mungu wako”(Kumb.5:16).

Yule anayewapenda wazazi na kuwaheshimu hawezi kuwasahau. Lazima atawafuatilia na kuwasaidia kuwashukuru kwa kumfanikisha. Kumbuka wakilalamika hautakuwa salama. Wao wanateseka na wewe unaishi kwa kustarehe, hiyo ni mbaya kabisa na ipo adhabu mbele yako!

Wengine hudiriki kusema sina wazazi kumbe siyo kweli. Tatizo lake ni kwamba eti atawatambulishaje wakati ni choka mbaya? Anaona bora wabaki huko vijijini ili isijulikane ana mzazi.

Mzazi anaweza asitamke neno kulaani lakini masikitiko yake na manung’uniko rohoni yakawa laana tosha! Hakuna mzazi anayependa kumlaani mwanae hata mmoja, lakini yanatokea tu anapokea laana bila sababu.

Mtu atasema mambo hayaendi, ndoa mgogoro, watoto ni shida changamoto ni nyingi. Eti huu ni mwaka mbaya, kumbe ipo laana juu yake kwa kujisahau katika jambo fulani, hivyo kusababisha yote hayo. Chunguza kabla ya kulaumu utapata majibu.

Vipo visa mbalimbali vinavyotokea katika maisha ya watu wengi, wengine wamewatangazia mambo ya uwongo wazazi wao. Hebu sikia kisa cha dada huyu;

Dada mmoja hapa Dar alikuwa akiishi kwenye kibanda kibovu jirani kabisa na ofisi za Serikali ya Mtaa akiwa na watoto wake wawili wadogo, miaka nane na miaka mitatu. Jumuia ya kinamama wa kanisa moja wakamchangia fedha Sh.200,000/= akapangishe chumba na aanzishe mradi mdogo kujikimu.

Akaondoka pale akahamia jumba linalojengwa jirani na kwangu. Nilipomhoji akasema anatafuta nauli arudi kijijini. Hakusema alishapewa hela. Nami nikampa Sh. 50,000 mbele ya mtendaji.

Nilipodadisi nikaambiwa kijijini hawezi kurudi kwani alikuwa akiishi na mamaye akamsingizia mchawi analoga wanawe. Mama alikanusha mbele ya uongozi wa kijiji lakini alipoona binti amemkomalia, akakoroga sumu akanywa na kufa.

Hiyo ndiyo laana inayomtafuna dada kwa kumsingizia mamaye ni mchawi. Ndio chanzo kuzurura mjini na wanawe kwani kijijini hatakiwi. Wiki ijayo usikose ushuhuda wa kutisha laana ya daktari aliyemdharau mama yake. Una maoni,

**Kisa? Ujumbe 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tanzania ijiandae vyema kusukuma agenda yake kwenye COP27

MKUTANO wa COP27 (Conference of Parties 27) unatarajiwa kufanyika Afrika kwa mara ya kwanza katika jiji la Cairo, Misri mwanzoni mwa Novemba, mwaka huu. Katika mkutano huo, Zambia ni mwenyekiti kutoka nchi zinazoendelea.

Mkutano huo unajumuisha wakuu wa nchi mbalimbali duniani zikiwamo nchi kubwa na ambazo zinaongoza katika kuzalisha hewa ukaa na kuchangia mabadiliko ya tabianchi.

Pia nchi za Afrika zinahudhuria na kila moja itatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ambayo kitaalamu inafahamika kama ‘National Determined Contribution’ (NDC), ambayo inaonyesha jitihada za kukabili na kukubali mabadiliko ya tabianchi kwenye kila sekta.

Kila nchi inasema malengo yake ya kupunguza hewa ukaa kwenye anga kwa kiasi gani kufikia mwaka gani. Mathalani, Tanzania imesema ikifika mwaka 2030 itapunguza hewa ukaa kwa asilimia 30 na kila sekta imefafanuliwa itawezeshaje kufikia malengo hayo.

Afrika inachangia asilimia 0.04 ya hewa ukaa duniani na nchi zinazoongoza ni Marekani na China ambazo zimewekewa malengo mahususi ambayo wakati mwingine yanashindwa kufikiwa kutokana na nguvu ya kiuchumi kwa kuwa viwanda vinaongoza kuzalisha hewa ukaa.

Mwananchi wa kawaida anaweza kujiuliza kwani mabadiliko ya tabianchi yananihusu nini? Hakuna ambaye mabadiliko haya hayamwathiri. Tukianza kwenye mvua za uhakika, kwa sasa hakuna na zikinyesha hazitoshelezi mahitaji ya kuzalisha chakula.

Tunashuhudia mvua kubwa kupita kiasi zenye madhara makubwa kwa binadamu, miundombinu na ardhi kwamba sasa udongo unazolewa na maji ya mvua kwenda maeneo ya tambarare na kuacha ardhi ikiwa tupu.

Aidha, kuna ongezeko la magonjwa kama malaria ambayo yanasababishwa na kuongezeka kwa mbu. Pia mimea inakumbana na magonjwa vamizi na mwisho watu kukosa chakula.

Pia maji yamepungua kiasi cha kuwa na ushindani wa kugombea rasilimali hiyo baina ya binadamu,mifugo na wanyama wafugwao,sasa migogoro inaongezeka baina ya makundi hayo. Tunaona wanyama wanakufa kwa kukosa maji na malisho.

Kwa sasa tunaona mikoa ambayo haikuwa na joto sasa ina joto jingi na mingine baridi kali kiasi cha barafu kudondoka. Yote haya ndiyo mabadiliko ya tabianchi kwamba dunia haiko kama ilivyokuwa awali au ilivyotakiwa kuwa tangu kuumbwa kwake.

Mjadala mkubwa duniani ni usalama wa chakula ambao unapungua siku hadi siku huku bei zikiendelea kupaa, mathalani nchini tunashuhudia nafaka zikipaa bei na kuadimika lakini kile kinachopatikana hakina ubora unaotakiwa.

Kama haitoshi, kwa sasa ardhi haina uwezo wa kuzalisha chakula bila kutumia mbolea za kemikali ambazo zinaingia kwenye maji ambayo hutumiwa na binadamu.

Kuna nchi hali ya ukame ni kali sana kiasi kwamba watu wanakufa. Kwa mfano, kaskazini mwa Kenya hali ni ngumu,na ndio maana Rais wa nchi hiyo, Dk. William Ruto akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), aliomba hatua madhubuti kunusuru nchi za Afrika.

Nchi za Afrika zinakabiliwa na changamoto nyingi na bahati mbaya zimekuwa wahanga wa mabadiliko ya tabianchi. Kabla hazijamaliza kushughulikia matatizo yaliyopo enzi na enzi kama umaskini, hazijasahau majeraha ya COVID-19 sasa zinakumbana na janga endelevu ambalo ni athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Tabia na ubinafsi wa binadamu ndiyo kumefikisha hali kuwa ilivyo sasa,bahati mbaya Afrika imetunza vyema misitu yake lakini ndiyo inabeba mzigo mzito wa mabadiliko hayo.

Sasa tunakwenda COP27 tena inafanyika kwenye ardhi ya Afrika. Pamoja na mambo yote tunataka kuona viongozi na watumishi wa serikali watakaokwenda huko wanatuwakilisha vyema.

Natambua kwenye mkutano mkubwa kama huu unaoleta maelfu ya watu kutakuwa na vikao vingi vya ndani na wazi. Ni muhimu watumishi wetu watakaokwenda huko kuhakikisha wanasukuma mbele agenda za nchi kwenye mabadiliko ya tabia nchi.

Lazima kusimama imara kuhakikisha nchi inanufaika na isiwe mwathirika tu wa mabadiliko ya tabianchi. Natambua tayari tuna NDC ngazi ya taifa ambayo inapaswa kushushwa hadi ngazi ya familia.

Ni matumaini yangu kuwa mkutano huo hautakuwa safari ya kutanua kwa watakaokwenda bali kuwakilisha nchi na vipaumbele vya nchi, kusukuma agenda za nchi na kuweka maslahi ya watanzania mbele.





Ilikuwa siku ya furaha kwa Bwana Harusi Mohamed Mchome, alipofunga ndoa na . Mwajuma Yakub. Ndoa hiyo ilifungwa Septemba 18 mwaka huu na kufuatia sherehe hiyo iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Simba Oil ulioko Mburahati, jijini Dar es Salaam.







MITINDO

# MIILI ILIYOJENGEKA Kila vazi linapendeza

UNAPOFIKIRIA kuhusu kupangilia mavazi ni muhimu kuzingatia aina ya mwili ulionao ili kukupa mwonekani mzuri.

Mwili wa kiume uliojengeka ni pendekezo zuri zaidi katika uvaaji wa nguo.


Wataalam wa mavazi wanashauri kwamba, kuvaa vizuri au kununua nguo maridadi haitoshi, lazima pia uhakikishe uonekane mwenye umbo zuri na linalovutia.

Ni muhimu kufanya mazoezi ya kujenga mwili, huku ukiwa mbunifu wa kupangilia nguo zako kuanzia suruali, mashati, fulana, viatu na mapambo mengine.

Unapovaa nguo inapendeza zaidi kama zitakupa nafasi ya kuonyesha baadhi ya viungo, kama mikono, kifua au tumbo.

Miili ya kawaida sio kama hautapendeza kuvaa nguo safi, lakini lazima uwe na sifa kadhaa za uvaaji ili kukupatia mwonekano maridadi.

Wanaume warefu waliojengeka vyema wanapovaa nguo zenye usawa wanazidi kuonekana na mvuto zaidi. Jambo la muhimu ni lazima kuvaa nguo zenye mgawanyiko sawa juu na chini kwa ajili ya kukuweka katika mtazamo wa kuvutia.









## UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# TENGENEZA USO NYUMBANI

NGOZI inatakiwa kujitengeneza yenyewe na si kuitengeneza kwa vipodozi kama wengi wanavyodhani.

Unaweza kuwa nyumbani mwisho wa wiki ukatengeneza uso wako na ukaendelea kuonekana mrembo.

Unaweza kutumia vitu vya asili ambavyo vinapatikana nyumbani au dukani ukaweka sawa uso wako na ukabaki kuwa mrembo zaidi.

Namna ya kutengeneza uso

Kwanza kabisa chukua maziwa ya mgando na utumie kusafisha uso wako. Upake kuanzia chini ya kidevu kupanda juu ya uso.

Fanya scrub kwa kutumia mchanganyiko wa mlozi na karoti au mlozi wa jani la chai.

Baada ya hapo anza kujikanda na maji vuguvugu yaliyochanganywa na kipande cha limao kidogo, chukua taulo la pamba na futa uso sehemu zote zenye tatizo.

Tumia ute mweupe ambao utakuwa umemwagia katika taulo lako na kujisugua taratibu.

Kadhalika jisafishe na maji ya vuguvugu.

Jikande tena kama ilivyokuwa katika hatua ya tatu juu.

Ili kuondoa ukavu wa ngozi, kata matango na yabandike katika ngozi.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Vyakula vinavyopunguza mwili

KUPITIA kona yetu ya mapishi wiki mbili mfululizo tulieleza maajabu ya vyakula vya kupunguza mwili wenye uzito mkubwa.

Leo tunaendelea kukueleza baadhi ya vyakula vitakavyokusaidia kupunguza mwili wako na kuwa na afya njema.

**SALADI**

Anza mazoea ya kutengeneza kachumbari yenye vitu mbalimbali iliyochanganywa na chakula cha protini kama yai la kuchemsha au nyama,samaki na maharage yaliyobaki usiku.

Uzuri wa saladi, kwanza zinashibisha sana kutokana na mboga mbichi pamoja na protini utakayoongeza.

Huokoa muda kwasababu ni rahisi kuandaa hata kama haujui kupika unaweza kutengeneza salad tamu sana!.

**OATSI**

Kifungua kinywa Kingine kinachosaidia kupunguza uzito ni Oats.

Hizi ni nafaka ambazo huwa hazijakobolewa kwahiyo hukaa tumboni muda mrefu pia hivyo kukupa hisia ya kushiba na kukuzuia kula sana.

**JINSI YA KUANDAA OATSI**

Unaweza kuloweka oats pamoja na vipande vya tunda, karanga na mbegu mfano ndizi, almonds au karanga na mbegu za chia.

Kwa kawaida unatakiwa kuloweka kwa kuchanganya oats, maziwa, karanga, chia seeds na matunda kisha kuhifadhi kwenye friji kwa ajili ya kula asubuhi kama kifungua kinywa.

Unaweza kupika oats kama uji kwa kutumia maziwa badala ya maji na maziwa kisha kuweka chumvi kidogo au vipande vya tunda tamu.

**NAFAKA ZISIZOKOBOLEWA**

Hizi husaidia kupunguza uzito kiasi fulani ila sio sana kama vyakula visivyo na kiasi kikubwa cha wanga.

Mara nyingi hapa ni pakuanzia kwa wale watu ambao wanapata shida kuacha au kupunguza vyakula vya wanga.

Mfano mzuri ni mkate wa brown na chapati za atta.

Nafaka zisizokobolewa husaidia kupunguza uzito kwa sababu hushibisha zaidi kuliko nafaka zilizokobolewa kutokana na kiasi chake kikubwa cha nyuzi nyuzi au fibre kutoka kwenye makapi ya nafaka hizo.



Kwa hiyo lazima utaona mabadiliko katika uzito wako pale utakapobadilisha vitafunwa vyako kutoka kwenye ngano nyeupe kuja kwenye ngano aina hii.

Kumbuka kwamba ukitaka kupungua vizuri na kwa kasi nzuri inabidi upunguze wanga na uongeze protini.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# MSIMU wa kupanga nyumba sasa unakaribia, usikurupuke

MSIMU wa kutafuta nyumba za kuishi unakaribia, hivyo ni vyema katika kipindi hiki ukawa makini zaidi katika kutafuta nyumba ambayo haitakuletea shida. Kwa maana hiyo, hakikisha haukurupuki kutafuta nyumba yenye hadhi yako na yenye usalama ili usije kujuta baadaye.

Hakikisha unazingatia mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kupanga nyumba kwa ajili ya kuishi.

Moja ya mambo ya kuangalia ni mahali nyumba ilipo na umbali. Kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi, lakini ikawa iko mbali zaidi au ikakulazimu kutumia pesa zaidi kwa upande wa usafiri.

Endapo unatumia usafiri wa umma, ikakulazimu kila ukifika kituoni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo, ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo. La sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kuangalia kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba zinaonekana vizuri kwa nje lakini ndani zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea. Kwa hiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe.



Lingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba, hawasemi ukweli na badala yake baada ya kulipia na kuanza kuishi ndipo huanza kuyasema kidogo kidogo kwa wapangaji, hivyo ni vyema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.

Hakikisha unausoma kwa makini mkataba kabla ya kulipia pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya, lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia mkataba wako unausoma vizuri. Kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza anafanya hivyo, kama ilivyo kwako.

Pia iwapo utabaini kama kuna kitu kinakufunga, ni bora uulize mapema kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.

Kadhalika, msimu wa mvua unakaribia, hakikisha unazingatia endapo eneo la nyumba ilipo hapajai maji kwa sababu hilo nalo ni jingine linaloweza kukuletea shida.

## Namna ya kusafisha uchafu juu ya dari



KATIKA kuweka mandhari nzuri ya jiko ndani ya nyumba ni lazima chumba kiwe na dari inayopendeza na inayong'aa.

Kufanikisha mazingira ya usafi jikoni, ni muhimu kuangalia rangi ya dari kama imechafuka au la, Kama imechafuka ni muhimu kusafisha ili kurudi katika hali yake ya kawaida.

Hizi ni baadhi ya dondoo muhimu wakati wa kusafisha dari.

1: Andaa vitu muhimu kwa ajili ya kusafisha dari kama fagio, kitambaa maalum ili kuepuka michirizi


2: Maji ya moto kwa ajili ya kuondolea uchafu mgumu ulioganda juu ya dari.

3: Poda maalum ya kuoshea kwa ajili ya kuepuka alama baada ya kusafisha.

4:Vipande vidogo vya sabuni kwa ajili ya kusafishia sehemu zilizokuwa na ukungu wa kupikia.

5: Tumia kifaa cha kusafishia madirisha kwa ajili ya kuondoa uchafu juu ya dari.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
WANAKUJA WAPO KAMA AROBAINI!
PANYA AU PAKA?
SI USEME NI AKINA NANI TUNA-RUSHANA ROHO!
UKINIACHILIA NAMUUA RASMI... WALIANZAJE HADI AMPE LIMBWATA MKE WANGU AJE KUNILISHA!
BABY MUACHE ANAHAMU NIMGEUZE GULUGUJA AKAMATIE UKUTA
UBABE UBABE... UNDUNDU[ UNDUNDU.. UNASHEMAJE?
IKO GUMI YA NANDONGA KUSAKUMBANA NAYO?
SHETANI ANA NGUVU KUSHINDA WANAOSHINDA 'JIMU' NAJISHANGAA MIMI NYUMBA SINA LAKINI MAFAO YANANISUKUMA NIJENGE HUKU NIAMBULIE MIBUSU!
SMOLU HAUSI
KAKA ULE MCHANGO NILIOKUCHANGIA SHEMELA NDIO HUYU?
HUKO KWAO KASHINDA MASHINDANO YA ULIMBWENDE NI MISS...
KABLA SIJAVUNJA HIZO NGWALA ZAKO NAMBIE KWA NINI UMEONEKANA GESTI MCHANA!
NILIKUWA NATESTI KAMA HABARI ZITA-KUFIKIA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MCHAWI KAROGWA KWELI...

HABARI KIMATAIFA

## Rais Benki ya Dunia agoma kujiuzulu

**GENEVA,** Uswisi

RAIS wa Benki ya Dunia David Malpass, amesema hatajiuzulu baada ya kuibuka kwa ukosoaji mkali dhidi ya matamshi yake aliyoyatoa kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Malpass mapema wiki hii alishindwa kutoa jibu la moja kwa moja alipoulizwa iwapo utoaji wa nishati ya mafuta umechangia ongezeko la joto duniani na badala yake alisema yeye si mwanasayansi.

Kwenye mahojiano na gazeti la Politico Friday la juzi, Malpass alisema hatajiuzulu na wala hajaombwa kufanya hivyo na serikali yoyote mwanachama wa Benki hiyo. Malpass aidha alisema Benki ya Dunia inachukua hatamu ya uongozi katika masuala ya hali ya hewa na kuongeza kuwa ni wazi nishati ya mafuta inayotokana na shughuli za binadamu huchangia mabadiliko ya tabianchi.

**DW**

## Canada yapigwa kimbunga Fiona

**OTTAWA,** Canada

ENEO la Mashariki mwa Canada linajiandaa kukabiliana na dhoruba kali zaidi ya kimbunga kuwahi kutokea katika historia ya nchi hiyo.

Kimbunga hicho kinachojulikana kwa jina la Fiona kiliingia kwa kasi katika eneo la Nova Scotia mapema jana.

Kulingana na kituo cha taifa cha Marekani kinachofuatilia vimbunga NHC, kimbunga Fiona kitaathiri baadhi ya sehemu za ukanda wa Atlantiki nchini Canada kikiambatana na upepo mkali, mawimbi ya dhoruba na mvua kubwa.

Waziri Mkuu wa Canada Justin Trudeau, alilazimika kuchelewesha ziara yake nchini Japan jana ambako alitarajiwa kushiriki mazishi ya waziri mkuu wa zamani aliyeuawa Shinzo Abe.

Mamlaka nchini Canada zimetangaza hali ya dharura katika eneo la Nova Scotia na kisiwa cha Prince Edward, na kutoa onyo la mafuriko makubwa kando ya fukwe. Watu wanaoishi maeneo ya pwani wameshauriwa kuhama makazi yao.

**DW**

# Marekani yapinga kura ya maoni Ukraine

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden amesema kura ya maoni ya Russia inayolenga kuyanyakua maeneo manne inayoyakalia nchini Ukraine kuwa haikubaliki.

Kiongozi huyo katika taarifa yake iliyotolewa jana, amesema maamuzi yoyote ya kuyatwaa maeneo hayo haitatambulika, vinginevyo maeneo hayo yabaki kuwa mali ya Ukraine.

Biden alisema watashirikiana na washirika wake kuongeza vikwazo zaidi vitakavyoiumiza Russia.

Hata hivyo, Rais Volodymyr Zelensky wa Ukraine, kwa upande wake ameutolea mwito ulimwengu kulaani kura hiyo wakati mawakala wa Russia wakiwa wameanza kupiga kura ya kunyakua maeneo hayo ambayo yalinyakuliwa.

Katika hotua zake za kila siku kwa taifa, Zelensky alisema majimbo manne nchini Ukraine ambayo yanadhibitiwa kwa sehemu au kikamilifu na Russia ya Donesk, Lugansk, Kherson na Zaporizhzhia, kusini mwa Ukraine ndiyo yanayopigiwa kura ya iwapo yanaweza kuchukuliwa moja kwa moja ama la.

Zelensky aliwataka wakazi wa maeneo hayo ambao wameandikishwa katika jeshi la Russia kuhujumu shughuli zozote za kijeshi.

"Fanya jambo la msingi kuokoa maisha yako na utusaidie kudhoofisha na kuwaangamiza wavamizi," alisema katika sehemu ya taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao wa Telegraph.

Aliongeza "Ficha kutoka kwa uhamasishaji wa Kirussia kwa njia yoyote. Epuka barua za kujiandikisha na jaribu kufika eneo huru la Ukraine.

Ikiwa tayari unaingia kwenye jeshi la Russia, basi hujumu shughuli yoyote ya adui, kuzuia shughuli zozote za Russia tupe habari yoyote muhimu kuhusu wavamizi na kambi zao, makao makuu, maghala na risasi. "

China ambayo imekuwa mshirika wa karibu zaidi tangu kuanza kwa vita vyake na Ukraine, ilikiri kwamba uhuru na utulivu wa eneo unatakiwa kuheshimiwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, alitoa matamshi hayo kwa mwenzake wa Ukraine Dymitro Kuleba, kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa juzi Ijumaa.

Katika hatua nyingine, Ukraine ilisema jana kuwa itapunguza uwepo wa ujumbe wa kidiplomasia wa Iran nchini humo baada ya kumpatia silaha hasimu wake Russia.

Taarifa ya wizara ya mambo ya nje ilisema Ukraine imeamua kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya watumishi kwenye ubalozi wa Iran ulioko Kyiv.

Mapema jana, Ukraine ilisema imezidungua ndege nne zisizotumia rubani zilizotengenezwa Iran, zilizoushambulia mji wa bandari wa Odessa, hatua iliyosababisha rais Volodymyr Zelensky kuilaumu Tehran kwa kuwadhuru raia na uhuru wake.

Ukraine na Marekani wameishutumu Iran kwa kuwapelekea Russia ndege hizo zisizo na rubani, shutuma ambazo zilipingwa vikali.

Sehemu ya taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya wizara hiyo ilisema "Kuipatia silaha Russia ili kupigana vita dhidi ya Ukraine ni kitendo ambacho si cha kirafiki, na kimeathiri uhusiano kati ya Ukraine na Iran".

Ujumbe huo umekabidhiwa kwa kaimu balozi wa Iran nchini Ukraine kwa kuwa balozi wa kudumu Manoucher Moradi hayupo nchini humo kwa sasa.

Katika hatua nyingine, Umoja wa Ulaya umepeleka barua kwa Umoja wa Mataifa ikiutaka kuchapisha ripoti inayoonyesha uharibifu wa miundombinu ya mawasiliano nchini Ukraine tangu Russia ilipoanzisha uvamizi wake nchini humo miezi saba iliyopita.

Mwezi Aprili, wanachama wa muungano wa kimataifa kwenye masuala ya mawasiliano ITU walipitisha azimio la kukubaliana kuisaidia Ukraine kujenga upya sekta yake ya mawasiliano.

**DW**



Maofisa wa polisi wanamshikilia mwanamume mmoja kufuatia wito wa kupinga uhamasishaji wa kujiunga na jeshi uliotolewa na Russia kwa ajili ya kwenda kupigana Ukraine. Zaidi ya watu 1,300 wamekamatwa kwenye maandamano yaliyofanyika sehemu tofauti nchini humo. **PICHA: AFP**

# Waliokufa Ebola wafikia watu 11

**KAMPALA,** Uganda

WIZARA ya Afya nchini Uganda imesema jumla ya watu 11 wamefariki dunia kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola nchini humo.

Taarifa ya wizara hiyo iliongeza kuwa hadi kufikia jana jioni watu wengine 11 wameambukizwa virusi vya ugonjwa huo hatari. Mamlaka za afya pia zinawafuatilia watu wengine 58 ambao walikaribiana na wale walioambukizwa. Kufikia siku ya Jumanne wiki hii, wizara ya afya ilikuwa imethibitisha kifo cha mtu mmoja pekee. Mlipuko wa Ebola ulitangazwa wiki hii kutokea katika wilaya ya Mubende nchini Uganda. Maambukizi ya ugonjwa huo mara nyingi husababisha homa kali na kutokwa na damu ndani. Uganda imekabiliwa na milipuko kadhaa ya Ebola, na mlipuko mkubwa ulianza mwaka 2000 ambao uliwaua zaidi ya watu 200 na kuambukiza wengine mamia katika sehemu za kaskazini mwa nchi.

**DW**

## SAFU

### MAKALA

# UKOSEFU WA AJIRA KISIWE KISINGIZIO



Na Magabilo Masambu
0689157789
magabilomjalifu@gmail.

KWANZA nakubaliana na wote wanaotoa maoni kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa. Kukubali kwangu ni kwa sababu kila mmoja wetu anayo haki ya kimsingi kabisa kwa mujibu wa Katiba kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 8 ya Katiba ya nchi yetu. Kama ambavyo mimi nina haki hiyo, ndivyo ilivyo kwa wengine. Lakini pamoja na uhuru huo, tunaweza kutofautiana katika kuyatazama mambo yenyewe. Nimesikiliza maoni ya baadhi ya watu kuhusu masuala ya kiuhalifu nchini mwetu, hasa kuhusu kundi la vijana wanaojiita Panya Road na makundi mengine. Wako wanaosema kwamba tatizo kubwa ni vijana hao kukosa ajira au kazi za kufanya. Inawezekana ni kweli lakini kwa maoni yangu nafikiri kama ni kweli basi ajira itakuwa sehemu ndogo sana tukilinganisha na ukubwa wa tatizo.

Malalamiko ya ukosefu wa ajira hasa ni juu ya vijana wengi wanaohitimu ngazi mbalimbali za elimu nchini na wanabaki mtaani. Lakini sote ni mashahidi kuwa vijana wanaofanya matukio ya kihalifu, wengi wao kama si wote, hawana viwango hivyo vya elimu. Baadhi yao utawasikia wanasema walikataa shule au waliishia darasa la saba na kadhalika.

Hatujasikia kuwa kwenye yale makundi wako wenye shahada, stashahada au astashahada ili tuamini kwamba wanafanya hivyo kwa sababu ya kukosa ajira. Sina maana kwamba wale wote ambao hawakusoma shule kwamba hawana haki ya kuajiriwa, ziko ajira za vibarua viwandani ndo kusema kama tungalikuwa na viwanda basi baadhi yao wangeliajiriwa huko japo pia wasingekuwa ni wote.

Suala la msingi ni lazima tujitafakari kama jamii hasa katika suala la malezi. Tusikwepe majukumu yetu ya kuwalea watoto katika misingi inayotakiwa badala yake tunaposhindwa kufanya hivyo, tunairushia lawama serikali kwamba haitoi ajira ndiyo maana watu wanakuwa wahalifu.

Sikatai na wala mimi si msemaji wa serikali na lazima ilaumiwe kwa sababu inayo mamlaka ya kisheria ya kuhakikisha usalama wa watu na mali zao, lakini mambo mengine tusaidiwe kwa kuchukua nafasi yetu kama wazazi na jamii kwa ujumla. Yuko mtu mmoja aliwahi kusema "Ukitumia gharama kubwa kulinda na kutetea makosa ya mwanao, ipo siku utatumia gharama kubwa vilevile kuwalipa mawakili mahakamani ili wamtetee mwanao dhidi ya uhalifu." Tuache hizi blablaa za kusema ohoo serikali ndiyo tatizo kwani ndiyo inayowazaa na kuwalea watoto wetu? Tunawazaa wenyewe, tunashindwa kuwalea kisha wakishakuwa wahalifu na pengine wakapata madhara kutokana na uhalifu wao tunarusha lawama.

Watoto hawawezi kuwa Panya Road kama wana malezi mazuri ya wazazi. Hakuna mhalifu anayeanza kufanya madhambi kwa jirani kabla ya kuanzia nyumbani. Wako wanaosema ohoo mimi hapa kwangu sjawahi kuona anaiba. Uhakika nilio nao ni kwamba amewahi kuiba nyumbani hapo, pengine hukuwahi kushitukia anaiba nini. Watoto wengine tunawaharibu wenyewe. Mtoto unataka kumtuma mahali eti anakupa masharti, kwamba ili aende ni lazima umpatie pesa alah! Watoto wadogo wako shule tunawazoesha pesa, mtoto yuko awali unampatia Sh. 1,000 ya kula shuleni. Yuko kidato cha kwanza unampatia Sh. 5,000 akale! Kidogo kidogo anazoea fedha mwisho wa siku hatasoma. Atapenda pesa zaidi, hivyo siku akizikosa kwako anatamani akaibe mwisho wa siku akipata kampani anaingia kwenye panya road, halafu usivyo na aibu unaanza kurusha lawama kwa wasiohusika. Ukiwa na watoto ndani ukaacha Sh. 50 mezani usipoikuta lazima uulize ilikokwenda, maana kesho wakikuta Sh. 10,000 wanachukua. Kuna tabia tunazijenga taratibu baadaye zinaleta matatizo makubwa. Kama hatuna uwezo wa kuwalea watoto, tusiwazae kwa sababu mwisho wa siku watapata matatizo ikiwamo kuuawa.

Nakubali wako ambao hawana wazazi pengine walishafariki dunia. Hao wazazi hawakuwa na ndugu? Unaachaje kulea watoto wa nduguyo, maana ukiwalea vyema iko siku watakusaidia na hii ni kwa sababu watoto wana tabia ya kujenga mapenzi na watu wanaokuwa nao karibu.

Mtoto hawezi kukupenda tu kwa sababu ulimzaa, bali kwa sababu umekuwa naye karibu toka utoto, ndiyo maana utasikia kesi za watoto kuwakataa wazazi wao japo kimaadili na kitamaduni haileti picha nzuri na huwa inatengeneza laana kizazi hadi kizazi, tunapojiweka mbali nao hawahisi kabisa kama huyu ni mzazi wangu.

Wako watu wana maisha magumu sana lakini hujawahi kusikia wakikaba kwa sababu walilelewa vizuri. Migogoro ya ndoa inayosababisha watoto kuanza kujitegemea wakiwa wadogo, nalo ni tatizo kubwa. Mama anaishi Kilimanjaro baba Dar es Salaam, watoto wako Manyara ni tatizo kubwa. Wako watoto wenye wazazi wote wawili, lakini wanaharibika kwa sababu mama na baba wanapishana katika kulea. Huyu anamwadhibu mtoto, mwingine anabembeleza kwa fedha, mmoja anaonekana mwema mwingine mbaya. Toto likiharibika, wanalaumiwa wote.

Viboko kwa watoto siku hizi vimekuwa adimu sana majumbani, eti tunalea kizungu! Sisemi malezi lazima viboko lakini tukubali, tukatae, maadili yameporomoka kwa sababu tumebadili mtindo wa malezi. Siku hizi bwana tunalea kisaikolojia! Mtoto akikosea tunambembeleza kwa fedha au vitu. Mtoto akiwa anatoroka kwenda banda la video, tunaona utatuzi ni kumnunulia runinga na deki awe anatazama chumbani kwake. Anaangalia nini hatutaki kujua, tunataka asitoke tu ndani lakini kwa kumpa anavyotaka, wakiharibika polisi hawafanyi kazi. Siku hizi watoto ndio wanatuendesha.

Mwisho, kama wazazi na jamii kwa ujmla turudi kwenye malezi jumuishi, zamani mtoto alikuwa wetu sote, siku hizi ni wangu. Akitukana huko barabarani akirudi nyumbani, tunampatia tuzo na pongezi, alafu wakianza kututukana sisi serikali haitoi ajira.

### BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Sikinde, Tomatoma wanatuambia michepuko tangu enzi ilikuwapo*



Na Adam Fungamwango

HAKUNA kitu chochote kinachofanywa kwenye kizazi cha sasa ambacho huko nyuma hakikuwapo. Kizazi cha sasa kinanufaika zaidi na teknolojia tu ambayo imekuwa kubwa sana na kurahisisha kazi na vitu vingi. Lakini kwenye maisha ya kawaida kwenye jamii, kila kitu kilikuwapo na watu walifanya zaidi kuliko wa sasa.

Watu wenye akili walikuwapo tangu enzi hizo na wengi wao ni wavumbuzi wa kila kitu, hata herufi hizi tunazotumia. Hata watu wenye roho mbaya unaowajua wewe hivi sasa hakuna kitu. Kuna watu walikuwa na roho mbaya miaka hiyo ya nyuma kuliko sasa.

Ndipo kulikuwa na hukumu za kunyonga watu hadharani, kuwambwa kwenye miti na hata kuchomwa moto, adhabu ambazo kwenye ulimwengu wa sasa hazipo tena. Dunia imestaarabika sana na sheria zinazowekwa sasa ni kwa sababu huko nyuma ilikuwa hatari sana. Mwenye nguvu aliweza kufanya vyovyote vile na asifanywe lolote.

Tunasikia eti kwa sasa watu wamebadilika hasa wanaume wamekuwa na wanawake wengi nje, maarufu kama michepuko.

Inawezekana ikawa ni kweli lakini ukiangalia sana unagundua kuwa hakuna kilichobadilika. Maisha ni yale yale tu. Hata zamani watu walikuwa na michepuko, si wanawake wala wanaume.

Hizi ni tabia za mtu binafsi, kwani kwenye maisha ya kawaida huwezi kukuta watu wanafanana tabia hata kama wamezaliwa baba na mama mmoja. Wakati hata zamani kulikuwa na watu wenye tabia njema na waadilifu, lakini ambao hawakuwa waadilifu nao walikuwapo.

Ushahidi wa hili upo kwenye baadhi ya nyimbo ambazo tunaziangalia hapa. Kwa kawaida wanamuziki hasa wa zamani walitunga nyimbo kutokana na kile anachokiona kikifanyika au kilichotokea ndani ya jamii. Ndiyo maana wakaitwa kioo cha jamii.

Tuanze na wimbo wa 'Edita' uliotungwa na Hassan Rehani Bitchuka mwanzoni mwa miaka ya 1980.

"Kipenzi changu Edita sikia ukweli niliokuwa nao, kusema kweli nimechoka na tabia yako. Ni siku nyingi nimelezwa mengi niliopuuza, nilijua ni fitina za majirani tu, wanataka kututenganisha. Lakini leo nimeamini, kipenzi Edita, methali ya Kiswahili yanena kwamba lisemwalo lipo. Nikitoka kazini sikukuti, nikuulizapo ulikuwa wapi? Nilikuwa kwa shangazi Kariakoo, kumbe una wako wa pembeni, kipenzi Edita. Hukuridhika mpaka umemleta kwako, wakati sipo niko kazini, waweza kuchukua kila chako, uende zako, kipenzi Edita."

Wimbo ni ushahidi tosha kwamba haya mambo yalikuwapo enzi na enzi na si kusema eti kizazi hiki cha sasa kimezidi. Kama dunia inaendelea na watu wanazidi kuzaliwa na kizazi kinakuja, kinaondoka na kuja kingine, haya yataendelea tu kwa sababu maisha ni mzunguko.

Hicho ni kisa cha mwanamke aliyekuwa akimzunguka mume wake na kumleta mchepuko wake ndani. Ni hatari sana na inaumiza. Lakini wimbo kama huu una funzo kubwa. Kuna watu wakipatwa na matatizo kama haya wanachukua uamuzi wa kujinyonga. Wanaona kama wamepewa aibu kubwa kiasi kwamba hawastahili kuishi na hasa wanaume ambao huumia zaidi.

Mtu anaona kwa nini imemtokea yeye tu na si mwingine, hivyo anachukua uamuzi mbaya. Kama kuna mtu amegundua kuwa mpenzi wake, mume au mke ana mchepuko, halafu akasikia wimbo kama huu kuwa afadhali yeye amegundua, lakini huyu amemfuma ndani kabisa, anaona kumbe afadhali yeye, kuna mwingine yalimkuta makubwa zaidi. Hapo hasira za kudhuru au kujidhuru hupungua.

"Kila siku mke wangu unarudi saa za usiku ufikapo nyumbani macho yau yau, nimevumilia sasa nimechoka, leo nataka unieleze ukweli, wapi unakochelewa.

Nachelewa stendi ya basi bwana ee, taabu ya mabasi waijua mume wangu, nihurumie bwana."

Wimbo huu unaitwa 'Stendi ya Basi' ulitungwa na Adam Bakari katikati ya miaka ya 1980 akiwa na Orchetra Tomatoma. Mke anachelewa kurudi nyumbani, mumewe akimuuliza anamwambia kachelewa stendi ya basi.

Hapa tunaona hata uongo nao unakwenda na wakati. Zamani kulikuwa na shida ya mabasi, akatumia uongo huo. Hivi sasa asingeeleweka. Mabasi yako mengi tu tena wanakaa mpaka foleni kusubiri abiria. Dada kwa sasa angesema kulikuwa na foleni ya magari. Uongo lazima uende pia na wakati.

Huyu alikuwa anachelewa kwa mchepuko wake, halafu anakuja 'kumfunga kamba' mumewe.

Hemed Maneti naye katikati ya miaka ya 1970 akiwa na Vijana Jazz, alitunga wimbo unaitwa 'Niliruka Ukuta'.

Jamaa ana mke, akakutana na mwanamke ambaye naye ana mume lakini amesafiri. Hapo kila mtu akawa mchepuko wa mwenzake. Mwanamke akamdanganya mwanamume kama hajaolewa, hivyo akaenda kwake. Kilichomkuta huko ni hatari tu.

"Nenda upesi nenda kamwambie, tokea leo asinifuatefuate, kitendo alichonitenda, kingenifanya nipoteze maisha. Kuniambia kwamba hajaolewa, na kile chumba amekipanga yeye, kumbe uongo amenidanganya, ilipofika saa nane ya usiku, nikasikia hodohodi fungua, bahati nzuri, nikaruka ukuta.Kama ukifika mwambie ajirekebishe, mambo kama yale mabaya na yana hatari. Kusema kweli si vibaya na wala dhambi, ya nini sasa kunificha na kunidanganya. Maisha yangu yangekwisha sababu ya yeye. Nimeponea chupuchupu nashukuru Mungu, kama si kuruka ukuta ingekuwa hatari."

Wimbo huu unaonyesha hasara ya michepuko, unaweza kudanganywa na kuingia mkenge, hivyo kuwa makini au salama zaidi ni 'kubaki njia kuu.'

**Tuma Meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-20

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

BABA yake alimuuliza baadhi ya maswali, lakini mengine alijibu kwa ujeuri, mengine hakujibu kabisa. Akahisi kitu. Alipoanza kupasuka maneno aliyoambiwa na Hidaya, ndipo mzee Pokwa alipojua kuwa rasmi sasa yote aliyoyaficha miaka mingi iliyopita, yamejulikana.

"Unataka kuniua kama ulivyomuua baba na mama yangu?"

"Tena afadhali yao, wewe nitakuua, halafu nakufukia humu humu ndani kama paka aliyeiba mboga. Huna hadhi ya kuzikwa kama binadamu wengine."

"Haina shida, siogopi kufa. Kama baba na mama yangu wamekufa, sembuse mimi waliyenizaa niogope, ila nataka unithibitihie kuwa ni kweli umefanya hivyo?"

"Kwa sababu umetaka mwenyewe na pia hata ufanyaje nini huwezi kutoka tena humu ukiwa hai, kila kitu ulichoelezwa ni kweli tupu." Pokwa alijitapa kwa dharau.

"Utalipa kwa ulichokifanya." Neno hilo lilisababisha kicheko kikali cha dharau kutoka kwa mzee Pokwa.


"Unajiamini sana kijana eee, ujanja wote na kazi hii nimekufundisha mimi, kwa hiyo niko mara 10 zaidi yako." Akamjibu.

Licha ya yote, bado Simon Pokwa aliendelea kushangaa ujasiri wa Prince, kwani pamoja na vitisho vyote, ambayo ni vya kweli, lakini hakuonekana kubabaika wala kuogopa.

"Lakini mtoto mdogo sana huyu." Akajiambia mwenyewe. "Saa zake na kuishi zinahesabika." Akaendelea kuwaza.

"Koba, njoo umalize mchezo, nimechoka kubishana na hiki kifaranga." Sauti ya mzee Pokwa ilisikika vizuri tu masikioni mwa Prince.

Ndipo alipogundua kuwa mzee Prince ni kweli alikuwa amejiandaa kumaliza siku kadhaa baada ya kumaliza kazi ya kuwaua wote aliowakusudia, kazi ambayo ilifanya na




**Ilikuwa ni sauti ya Prince ikimuamrisha mzee Pokwa, lakini papo hapo ikiambatana na sauti ya risasi ambayo iliipiga sawia kwenda kupiga mkono wake wa kulia uliokuwa na umeshika bastola.**

yeye mwenyewe, huku aliowaua walitakiwa wawe hai ili kumsaidia kwenye kesi ya mauaji ya wazazi wake pamoja na mali zake za urithi wa marehemu baba yake. Akaanza kunusa harufu ya mauti.

Ghafla aliona mtu akichomoza kama mzimu kwenye varanda ya nyumba hiyo akiingia kwenye sebule ukumbi wa kulia chakula.

Mafunzo ya baba yake huyo wa mchongo na mengine ambayo alijiongeza yalimfanya kuwa imara na makini wakati wote, hakusubiri aliruka pembeni alipokuwa amekaa kwenye kiti.

Sehemu aliyotoka tayari ilikuwa imetupia risasi mbili ambazo zingempata kama angeendelea kukaa pale. Alirukia kwenye kochi alilokuwa amekaa, lakini papo hapo akarukia sehemu nyingine, kochi nalo likichanwachanwa na risasi.

Kitendo hicho bila kuchelewa, alichomoa bastola yake kwani wakati akibishana na mzee Pokwa alijua lolote linaweza kutokea.

Kama umeme alifyatua risasi mbili kuelekea kule zilikokuwa zinamiminwa, lakini aliyekuwa akifanya hivyo alirejesha mwili wake kwenye ukuta uliotenganisha varanda na ukumbi. Zilikwangua ukuta. Wakati huo huo, Simon Pokwa na yeye alikuwa ameshatoa ya kwake. Naye alikuwa amechukua nafasi yake chini ya meza. Alijua anayepambana naye ni hatari kwa shabaha na amemfundisha mwenyewe.

Risasi tatu zilipita juu ya kichwa cha Prince, wakati huo akiwa amejificha pembeni ya kabati. Kwa uzoefu mdogo aliokuwa nao wa mambo hayo, hatari kwake alioona ipo zaidi kwa mtu yule asiyemfahamu kuliko mzee Pokwa.

Macho yake yote yalikuwa kwenye ukuta huo, ambao varanda na ukumbi vilitengenishwa na pazia yenye mtindo wa kuchanwachanwa, hivyo baadhi ya vipande vilikuwa vikipeperushwa na upepo.

Kwa umakini zaidi Prince, alikaza macho yake pale na haikupita sekunde 30, yule mtu alionekana kuchungulia ili kuona kama anaweza kumuona vema anayemuwinda.

Ndiyo muda aliokuwa anasubiri, kwani alifyatua risasi moja iliyompata vema kichwani. Kitendo hicho kilimfanya ayumbe na mwili wake kuingia ndani ya sebule. Akaongeza nyingine ya kichwa iliyomwaga chini kama mzigo.

Hakujidanganya kuwa vita imeisha. Alijua huenda kukawa na watu wengine nje, au sehemu yoyote inayofanana na hiyo. Pili alijua Pokwa anamuwinda na hatosita kummaliza kwa sababu tayari ameshajua ukweli wote ambao amekuwa akiuficha kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Kwa hiyo hakujitokeza. Ikawa ni kama watu wanaoviziana.

Dakika moja ilipita bila kusikika tena milio ya risasi iliyokuwa inaunguruma dakika chache zilizopita. Kwa ujanja alionao, Prince aliuona mfuko mdogo wa karatasi uliokuwa chini yake na ndani yake ulikuwa umewekwa vitu vidogo vidogo na kutuna . Kwa uangalifu, aliinama chini na kuuinua. Akaurusha katikati ya ukumbi. Alichokitaka ndicho kilichokuwa.

Mzee Pokwa, alidhani kuwa Prince ametoka alipojificha. Ghafla akajichomoa alipojificha kwa lengo la kumchapa risasi Prince. Badala yake akashtukia hakuna mtu, ila ni kitu kimerushwa. Akataka kurudi, lakini akawa amechelewa.

"Simama hivyo hivyo, ukirudi nyuma robo hatua tu, natawanya ubongo." Ilikuwa ni sauti ya Prince ikimuamrisha mzee Pokwa, lakini papo hapo ikiambatana na sauti ya risasi ambayo iliipiga sawia kwenda kupiga mkono wake wa kulia uliokuwa na umeshika bastola.

Pamoja na mkono wake kuvuja damu na kuonekana una majeraha yaliyoambatana na maumivu makali, mzee Pokwa bado hakukubali kirahisi.

"Hivi unadhani ndiyo utafanikiwa? Nimekwambia huwezi kuniua kirahisi, weka bastola yako chini usalimu amri, angalau naweza kukusamehe." Akasema kwa sauti ya kijeuri, hasira, kujiamini, lakini ikionekana kuwa ana maumivu.

Hilo pekee lilimfahamisha kuwa bado mzee Pokwa kuna kitu anategemea. Kwa hali ya kawaida angeweza kunyoosha mikono juu. Kengele ya hatari ikagonga kwenye kichwa cha Prince kuwa inawezekana ikawa bado yuko hatarini.

**Itaendelea Jumapili**



# CHRISTINA TOSSY ASISITIZA UPENDO

Siku chache baada ya kuachia wimbo 'Wewe Tu Unastahili', mwimbaji wa Injili, Christina Tossy, amesisitiza upendo baina ya waimbaji wa muziki huo.

Akizungumza na NIPASHE, Tossy, amesema kazi ya Mungu inahitaji ushirikiano hivyo ni vizuri kwa waimbaji kupendana na kushirikiana kwenye mambo muhimu.

"Natamani waimbaji tuzidi kupendana na kusaidiana kwenye kazi zetu ili tuzidi kufanya kazi ya Mungu. Binafsi nashukuru tangu nimeachia wimbo wangu 'Wewe Tu Wastahili' uungwaji mkono umekuwa mkubwa kwa mashabiki na waimbaji wenzangu," amesema Tossy.

# Man Mo, nyota inayong'aa kwa kasi

MOJA ya vijana wenye ndoto ya kufanya makubwa ni mtunzi na nyota inayochipukia katika muziki wa kizazi kipya, Maneno Mohamed, maarufu kama Man Mo.

Man Mo, mwenye sauti tamu inayochagizwa na uwezo wake wa kuandika mashairi mazuri, amesota muda mrefu katika kukuza jina lake, mpaka alipoibuliwa na Hayati Rais John Pombe Magufuli, alivyousifia wimbo wake unaoitwa 'Sweet Kitunguu'.

Tukio hilo analikumbuka katika maisha yake wakati Magufuli alipofanya ziara wilayani Kisarawe, mkoani Pwani na yeye alipanda jukwaani na kuimba wimbo huo.

Akizungumzia mafanikio ya kutajwa na aliyekuwa Rais huyo wa nchi Man Mo, amesema hawezi kusahau tukio hilo katika maisha yake kwa kutajwa na mtu mzito anayeangaliwa na wengi.

"Sina mafanikio makubwa, lakini angalau naweza kusimama na kusema kazi yangu ilikuwa kati ya zile zilizomkosha Rais wa nchi.

"Hii inanifanya nisikate tamaa, niendelee na mapambano kwa sababu najua maisha ya sanaa yanahitaji moyo na kufanya kazi bila kuchoka kadri unavyoungwa mkono na wadau mbalimbali wa sanaa nchini," alisema Mo.

Mo, anayetajwa kama moja ya wasanii wanaoweza kuandika vizuri mashairi, anakumbuka kwa mara ya kwanza alivyoweza kuandika wimbo mzuri wa Nasimama ulioimbwa na mkali Lady JayDee.

Kama wengine, Mo alianza kuangalia kwanza sanaa ya mama yake marehemu Salma Musa, kabla ya kuanza kujiingiza kwenye tasnia ya muziki wa Bongo Fleva.

"Mama yangu alikuwa mtu wa kwanza kumuona na kutamani kuingia kwenye muziki, licha ya kwamba alihusika na ngoma tu kwenye shughuli mbalimbali kijijini kwao," alisema.

Msanii huyo anawataja pia wakali wengine wanaofanya kazi nzuri ambao mpaka sasa anatafuta namna ya kufikia sehemu nzuri kama njia ya kutimiza ndoto zake.

Anautaja mwaka 2010, kuwa ndio alianza rasmi harakati zake za muziki kwa kuamua kuja jijini Dar es Salaam kwa ajili ya muziki wa kizazi kipya, licha ya kuwa alijichanganya katika shughuli mbalimbali ili mkono uende kinywani.

Studio za Sharobaro zilichangia pia kumuweka katika hatua nzuri kimuziki na kuandika nyimbo nyingi kama vile, Binti wa Kibara, Binti wa Kimasai, Nasimama na nyinginezo.

Baadaye alifika kwenye Studio za Classic Sound chini ya mtayarishaji wake Monagenster aliyempa nafasi mbalimbali, na kwamba hata wimbo wake Sweet Kitunguu alioutengenezea kwenye studio hiyo, akiwa chini ya utawala wake wa zamani ANE, (African Network Entertainment.



Mpaka sasa nyimbo za Man Mo, zilizofanya vizuri ni 'Tike, Mapenzi Kazi, Hamida na Sweet Kitunguu zilizofanya vizuri.

Mo yupo mbioni kuachia wimbo wake mpya uitwao Faraja, akitengeneza chini ya mtayarishaji wake Abidady.

Mo alizaliwa kwenye familia ya watoto wanne, huku yeye akiwa wa kwanza kuzaliwa mwaka 1994 huko Kimange, wilayani Chalinze mkoani Pwani.

## ZISIKUPITE

### TRAORE ANUKIA JUVENTUS

KLABU ya Juventus inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Wolves na Timu ya Taifa ya Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, wakati dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa. ***(Birmingham Mail)***

### ASSENSIO ATAJWA JUVE

JUVENTUS pia wanamtaka mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31, ambaye yuko kwa mkopo Atletico Madrid kutoka Barcelona, pamoja na kiungo wa kati wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio (26), na winga wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic (24). ***(Football Italia )***

### GRIEZMANN, BARCA SAFI

BARCELONA wanawania kukamilisha dili la pauni milioni 22 kwa ajili ya uhamisho wa kudumu wa mshambuliaji, Antoine Griezmann aliyeko Atletico Madrid. (***Mail***)

### MIRRETTI KUIKAMUA ARSENAL

ARSENAL wanaweza kuwekewa dau la pauni milioni 101 mara mbili ya uhamisho wa mshambuliaji wa Juventus, Dusan Vlahovic ambaye ni raia wa Serbia mwenye umri wa miaka 22 kwa kiungo wa kati wa Italia, Fabio Miretti (19). (***Sun***)

### ARSENAL YAMTAKA LINDSTROM

ARSENAL pia wamewasiliana na Eintracht Frankfurt kuhusu winga wa Timu ya Taifa ya Denmark mwenye umri wa miaka 22, Jesper Lindstrom. (***Mail***)

### CHALOBAH KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 23 amehusishwa na tetesi za kutaka kuondoka Chelsea huku AS Roma ya Jose Mourinho ikitarajiwa kumununua ifikapo Januari. (***Corriere dello Sport***)

### NICE YAMKANA POCHETTINO

KLABU ya Nice ya Ufaransa imekana kumlenga kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya, na inasemekana kumtaka kocha wa zamani wa Bournemouth, Scott Parker. (***Sun***)

### BAENA AGOMBEWA EPL

KLABU ZA Arsenal, Chelsea, Liverpool na Manchester City zinamfuatilia kiungo wa kati wa Hispania na Villarreal mwenye umri wa miaka 21, Alex Baena, ambaye ana kipengele cha kuondoka cha euro milioni 35. (***Sport***)

### CHELSEA, CITY VITANI

CHELSEA na Manchester City pia zinavutiwa na mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23 ambaye thamani yake inadaiwa kuwa zaidi ya pauni milioni 100. (***Evening News Manchester***)

### CONTE KUREJEA JUVENTUS

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte yuko tayari kurejea Juventus msimu huu iwapo Massimiliano Allegri atatimuliwa. (Star)

### HAZARD AHITAJI KUCHEZA

EDEN Hazard amezungumza kuhusu hali yake "tete" katika klabu ya Real Madrid na mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji mwenye umri wa miaka 31 anatamani kupata muda zaidi wa kucheza kabla ya kuanza kwa fainali za Kombe la Dunia. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KIWANGO CHA BRAZIL CHAMFURAHISHA TITE

## Ni katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Ghana ambapo...

**LE HARVE,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Brazil, Tite amesifu uchezaji "wa kuvutia" wa timu yake wakati ikiisambaratisha Ghana katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa juzi.

Timu hiyo ya Amerika Kusini iliibuka kidedea kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya wababe hao wa Afrika katika mechi hiyo iliyofanyika Ufaransa, Marquinhos akifunga bao la kwanza ndani ya dakika tisa na Richarlison kufunga mabao mawili kabla ya mapumziko.

Ushindi huo wa pale Le Havre, umeongeza matumaini kwa mabingwa hao mara tano wa Kombe la Dunia kabla ya michuano hiyo itakayofanyika baadaye mwaka huu.

Hata hivyo, Tite alifurahishwa na kiwango cha timu yake kwa kutafuta haraka mpira pale walipopoteza.

"Katika kipindi cha kwanza, timu ilijipanga na tulikuwa tukitafuta mpira haraka kila tukipoteza," alisema akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Kuna njia tofauti za kuiita: kupoteza-na-kurudisha. Lakini kasi yetu ya kumiliki tena ilikuwa ya kuvutia. "Mipira iliposimama, timu pia ilikwenda vizuri, ilikuwa safi. Kuja Ufaransa kumesaidia kubadilisha upepo.

"Kipindi cha kwanza, timu ilikuwa na kasi na mchezo, walitawala na kudhibiti. Kipindi cha pili, Ghana walifanikiwa kudhibiti kwa dakika 15, hatukuweza kuwamaliza kwani walikuwa na ukuta wa wachezaji watano," alifafanua.

"Wakati huo huo, tulikuwa imara. Kwa kuingia kwa wachezaji wapya (waliotokea benchi), tulipata utawala tena.

"Kisha tulipata nafasi za wazi za kuongeza uongozi wetu. Matheus Cunha alipata nafasi mbili za wazi, kulikuwa na nafasi kwa Neymar, Rodrygo na Paqueta.

"Kwa hiyo, timu iliweza kufanya vizuri katika hatua hizi tofauti, lakini kuwa sawa na kile tulichofanya katika kipindi cha kwanza haifanyi kazi kila wakati."

Brazil itamenyana na Tunisia keshokutwa katika mchezo wao wa mwisho wa kirafiki kabla ya kuelekea katika fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika kuanzia Novemba mwishoni.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
NETHERLANDS
VERSUS
BELGIUM
1 | 2.24
X | 3.54
2 | 2.94

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MANCINI: TUMEWAFUNGA, LAKINI ENGLAND INA NAFASI



**MILAN,** Italia

ROBERTO Mancini, alisifu kizazi kipya cha Italia baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya England katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa iliyochezwa juzi.

Goli la Giacomo Raspadori lililofungwa kwenye Uwanja wa San Siro liliifanya England ishushwe daraja hadi Ligi B ya michuano hiyo, wakati Italia sasa itamenyana na Hungary hapo kesho kuamua nani atafuzu kwenda kucheza fainali za Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Baada ya kushindwa kufuzu kwa Kombe la Dunia nchini Qatar, Mancini ameangalia wachezaji wachanga kwa siku za usoni huku Raspadori mwenye umri wa miaka 22 akiwa kivutio kikubwa kwa mabingwa hao wa Ulaya.

"Tulianza upya Juni na mara zote tulikuwa kwenye mbio za kundi hili la Ligi ya Mataifa ya Uefa. Ni wazi, tunahitaji michezo hii, ushindi huu, ili tuweze kukua," alisema.

"Nilitarajia utendaji mzuri na nilijua itakuwa ngumu, kwa sababu vijana wengi wa usiku wa leo (juzi) hawana uzoefu katika kiwango hiki, lakini nadhani tulishinda kwa kustahili."

Kisha Mancini, aliulizwa ni kwa nini Italia wanaonekana kuwa na ufanisi zaidi wanapokuwa chini ya shinikizo kuliko katika michezo ambayo wakuwa na nafasi ya kushinda.

"Sidhani, soka lina kitu cha bahati, tulishinda Euro kwa mikwaju ya penalti, tulistahili kushinda, halafu tukashindwa kufuzu Kombe la Dunia baada ya michezo miwili tuliyoitawala na hatukushinda, dhidi ya Uswizi," alieleza.

Kuhusu England, Mancini anabakia na imani kwamba, kikosi hicho cha kocha, Gareth Southgate kinaweza kuwa mshindani mzuri kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar.

# Flick akubali lawama kichapo cha Ujerumani



**LEIPZIG,** Ujerumani

KOCHA wa Ujerumani, Hansi Flick, amesema lazima awajibike kushindwa kwa timu yake katika Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Hungary, baada ya kupoteza kwa mara ya kwanza.

Bao la Adam Szalai kipindi cha kwanza lilikuwa pekee la kupoteza kule Leipzig, kwenye Kundi la A3.

Ujerumani ilipoteza kwa mara ya kwanza dhidi ya Hungary tangu mwaka 2004, huku kikosi cha Flick kikionekana kutokuwa kwenye ubora wake.

Mara baada ya mchezo huo, kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich alikiri timu yake ilicheza vibaya.

"Tulitaka kujaribu kitu, lakini hatukuwa kwenye uboraa," aliiambia ZDF.

"Lazima niwajibike kwa hilo. Hatukuwahi kufika pale tulipotaka kuwatumia."

Akizungumza na wanahabari muda mfupi baadaye, Flick aliongeza timu yake haitakatishwa tamaa na matokeo hayo huku Kombe la Dunia la Qatar 2022 likikaribia, akiongeza: "Kushindwa huku hakutatutupa nje ya mstari.

"Tunajua kile kinachohitajika kwetu sasa na hii imetufungua macho kidogo. Ni bora kupoteza sasa badala ya Kombe la Dunia.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

# CAG AANIKA UBADHIRIFU UWANJA WA AMAAN, ZBAR

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG), Zanzibar imebaini dosari ya kutotangazwa kwa zabuni ya wazi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ununuzi wa taa za Uwanja wa Amani zenye thamani ya Sh. milioni 270.

Aidha, ukaguzi haukupatiwa muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichompendekeza mzabuni huyo na kusababishwa wakaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo ikiwa ni kinyume cha kifungu 68(1) cha Sheria namba 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

CAG Dk. Othman Abbas Ali, alibainisha hayo kupitia ukaguzi uliofanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kwa kuzingatia misingi, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

"Ukaguzi umepitia mikataba na hati mbalimbali na kubaini wizara hii imetumia Dola za Marekani 119,000 ( sawa na Sh. milioni 270.2) katika ununuzi wa taa kutoka Kampuni ya Hong Kong Light Technology kwa ajili ya kiwanja cha Amaan," alisema mkaguzi huyo.

Aliongeza ukaguzi ulishauri uongozi wa wizara hiyo, uhakikishe unafuata kikamilifu sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma namba 11 ya mwaka 2016 wakati wa kufanya manunuzi.

Ripoti hiyo ilibaini pia upungufu katika ufungwaji wa mkataba wa ujenzi wa Uwanja wa Mkokotoni wa Sh. milioni 205.7, dosari iliyobainika na CAG katika ukaguzi huo ni kutokukamilika kwa mradi wa ujenzi huo kunakotokana na kukosekana kwa tathmini nzuri ya upembuzi yakinifu juu ya utekelezaji wa mradi huo na kusababisha kutokuwapo na tija katika mradi huo.

Ripoti ilionyesha ukaguzi ulitembelea miradi ya uimarishaji wa viwanja na kutambua mnamo mwaka 2020, wizara iliingia makubaliano ya kimkataba baina ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi akiwa ni mkandarasi na Wakala wa Majengo (ZBA) akiwa ni mshauri elekezi wa ujenzi wa kiwanja cha netiboli, wavu, mpira wa mikono na kikapu.

Aidha, ilibaini dosari katika ununuzi wa PA System ya Sh. milioni 84.9 kutokana na kutotangazwa kwa zabuni ya wazi kwa ajili ya kumpata mkandarasi.

Alisema katika ukaguzi huo, walibaini wizara hiyo ilitumia Sh. 84,908,050 katika ununuzi wa PA System za kiwanja cha Amani kutoka kwa Kampuni ya Rakam General Suply ltd.

Ukaguzi ulishauri uongozi wa wizara hiyo uhakikishe unafuata kikamilifu sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016 wakati wa kufanya manunuzi.



Mchezaji wa Timu ya Soka ya Vijana ya Taifa ya umri chini ya miaka 23, akipambana kuwania mpira dhidi ya mpinzani wake kutoka Sudani Kusini (kulia), katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-23), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: TFF**

INATOKA UK 24

## *Phiri afunguka Simba ilivyopania*

Straika huyo ambaye ana mabao matatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mawili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, amewapongeza pia viongozi na benchi la ufundi la timu hiyo kwa wazo lao la kutafuta mechi za kirafiki katika kipindi hiki cha mapumziko kupisha Kalenda ya FIFA.

"Si vizuri kukaa muda mrefu bila kucheza, kwa hiyo nawapongeza viongozi na benchi la ufundi kwa ziara hii ya Zanzibar kwa ajili ya mechi za kujipima nguvu, hasa kipindi hiki cha mapumziko," Phiri alisema.

Simba leo inatarajia kutumia nyota wake ambao wamebakia kikosini kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Malindi itakayochezwa kuanzia saa 2:00 usiku kwenye Uwanja wa Amaan.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili lengo la kucheza mechi ya leo na nyingine itakayofuata ni dhamira ya kukiimarisha kikosi chake kutokana na majukumu waliyonayo.

Wekundu hao wa Msimbazi watashuka tena dimbani Jumatano kuwakabili Kipanga ambayo pia inajiwinda na mechi ya raundi ya kwanza ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

INATOKA UK 24

## Yanga SC yachambua dakika 180 za CAF

"Tungependa kuona tunajiweka vizuri katika mechi ya kwanza, ingawa pia haitakuwa rahisi, lakini tumejipanga kisawasawa, tumezitazama mechi zao walizocheza dhidi ya St. George ya Ethiopia nyumbani na ugenini. Inabidi tubadilike kidogo, kuna wakati tunacheza tunakosa mabao mengi, kunashindwa kutumia nafasi tunazopata, katika mechi kama hiyo dhidi ya Al Hilal au zinazofuata ni ngumu, haiwezekani kupata nafasi nyingi kama tulizozipata dhidi ya Zalan FC, zitakuwa chache sana, hivyo zinapaswa kutumiwa vizuri," Kaze alisema.

Kabla ya mechi hiyo ya kimataifa, Yanga itakutana na Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Oktoba 3. mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 25/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5893 | Veles vs KamAZ | 2.26 | 3.14 | 2.95 |
| 14:00 | 5938 | Tegs SK vs Motala Aif | 6.67 | 5.29 | 1.31 |
| 14:30 | 4308 | Plymouth vs Ipswich | 3.10 | 3.30 | 2.20 |
| 15:00 | 1561 | FC Krasnodar II vs Neftekhimik | 2.80 | 3.25 | 2.40 |
| 15:00 | 2213 | Burgos vs Levante | 3.34 | 3.00 | 2.24 |
| 15:00 | 5615 | FK Karlskrona vs Hogsby IK | 1.72 | 3.70 | 4.40 |
| 15:00 | 5810 | Chengdu Qianbao vs Henan Jianye | 2.39 | 3.20 | 2.71 |
| 15:00 | 5971 | Osterlen FF vs FC Rosengaard | 3.43 | 3.68 | 1.86 |
| 15:45 | 3879 | Cliftonville Belfast vs Queens Park | 2.26 | 3.64 | 2.61 |
| 15:45 | 5718 | VSK Aarhus W vs Brondby W | 5.32 | 4.63 | 1.44 |
| 16:00 | 2881 | Moldova vs Liechtenstein | 1.19 | 6.20 | 13.00 |
| 16:00 | 4073 | Andorra vs Latvia | 4.40 | 3.40 | 1.78 |
| 16:00 | 4922 | Akron Tolyatti vs Ufa | 3.64 | 3.24 | 1.94 |
| 16:00 | 5788 | Radunia Stezyca vs PKS Olimpia Elblag | 1.75 | 3.48 | 4.12 |
| 17:00 | 2388 | Volgar Astrahan vs FC Alania Vladikavkaz | 3.67 | 3.23 | 1.93 |
| 17:00 | 2420 | Bray Wanderers vs Waterford Utd | 5.29 | 4.02 | 1.51 |
| 17:00 | 3370 | Croatia Zmijavci vs Orijent Rijeka | 2.10 | 3.21 | 3.21 |
| 17:00 | 4136 | EIF Ekenas vs Japs | 1.59 | 4.13 | 4.33 |
| 17:00 | 5495 | PK-35 vs Pif Jalkapallo | 1.41 | 4.51 | 5.88 |
| 17:15 | 4360 | Lugo vs Real Oviedo | 3.20 | 2.95 | 2.33 |
| 18:00 | 1088 | Olot vs Valencia B | 2.29 | 2.95 | 3.09 |
| 18:00 | 2222 | Sociedad Deportivo Tarazona vs SD Beasain | 2.07 | 3.10 | 3.39 |
| 18:00 | 2441 | Pontevedra vs Linense | 1.90 | 3.49 | 3.49 |
| 18:00 | 3121 | Marino Luanco vs Zamora CF | 2.11 | 3.24 | 3.14 |
| 18:00 | 3469 | CD Cristo Atletico vs Bergantinos CF | 2.26 | 3.04 | 3.04 |
| 18:00 | 4457 | Utebo FC vs Izarra | 2.31 | 2.91 | 3.10 |
| 18:00 | 5267 | JS Hercules vs OLS Oulu | 2.06 | 3.78 | 2.85 |
| 18:00 | 5814 | Alfaro CD vs Tudelano | 2.95 | 3.05 | 2.30 |
| 19:00 | 1175 | Fuenlabrada vs CF Talavera De La Reina | 1.42 | 4.31 | 6.08 |
| 19:00 | 1408 | Leonesa vs Cordoba | 3.39 | 3.58 | 1.90 |
| 19:00 | 2282 | SD Compostela vs UP Langreo | 1.67 | 3.48 | 4.71 |
| 19:00 | 2659 | UD Alzira vs CD Teruel | 2.85 | 3.10 | 2.47 |
| 19:00 | 4472 | CD Guadalajara vs AD Alcorcon B | 2.17 | 3.60 | 2.90 |
| 19:00 | 4551 | Yeclano Deportivo vs Velez CF | 2.47 | 3.10 | 2.85 |
| 19:00 | 4622 | Azerbaijan vs Kazakhstan | 2.27 | 3.13 | 3.23 |
| 19:00 | 5175 | Numancia vs CF La Nucia | 2.12 | 3.24 | 3.14 |
| 19:00 | 5609 | SD Gernika vs Racing Rioja CF | 1.92 | 3.34 | 3.59 |
| 19:00 | 5613 | CF Villanovense vs Leganes B | 2.33 | 3.25 | 2.75 |
| 19:30 | 1403 | Eibar vs Racing Santander | 1.59 | 3.60 | 5.80 |
| 19:30 | 3986 | Albacete Balompie vs FC Andorra | 1.90 | 3.34 | 3.94 |
| 19:30 | 4435 | Burgos Promesas vs Ourense CF | 2.12 | 3.04 | 3.34 |
| 19:45 | 3969 | Atletico Sanluqueno vs Recreativo Huelva | 1.95 | 3.87 | 3.04 |
| 20:00 | 1506 | Atl Mancha Real vs CD Utrera | 2.07 | 3.45 | 3.25 |
| 21:45 | 1420 | Faroe Islands vs Turkey | 8.60 | 5.00 | 1.30 |
| 21:45 | 3002 | Austria vs Croatia | 2.87 | 3.22 | 2.43 |
| 21:45 | 4595 | Wales vs Poland | 2.68 | 3.24 | 2.58 |
| 21:45 | 5436 | Luxembourg vs Lithuania | 1.63 | 3.55 | 5.40 |
| 21:45 | 5456 | Denmark vs France | 3.28 | 3.43 | 2.11 |
| 21:45 | 5540 | Netherlands vs Belgium | 2.24 | 3.54 | 2.94 |
| 22:00 | 4385 | Las Palmas UD vs Granada | 2.39 | 3.15 | 2.90 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Septemba 25, 2022

Nipashe




## Kiwango cha Brazil chamfurahisha Tite

HABARI UK 21



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Mohamed Matili (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Sudani Kusini katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Black Rhino ulioko Karatu, Manyara jana. **PICHA: TFF**

# Phiri afunguka Simba ilivyopania

**Adam Fungamwango na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

### Mzambia huyo aahidi ataendelea kuwafurahisha mashabiki kwa sababu...

STRAIKA ambaye hivi karibuni ameanza kuwateka wanachama na mashabiki wa Simba, Moses Phiri, amesema wachezaji wa timu hiyo wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanacheza vizuri, wanafunga mabao na kusaka ushindi katika kila mechi ili kuwafurahisha mashabiki wao ambao wamekuwa na mchango mkubwa kwenye mafanikio ya timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Phiri alisema anawapongeza sana wanachama na mashabiki kwa kuwapa sapoti kila timu inapokwenda, hivyo wanachostahili kupewa ni matokeo ya ushindi.

Phiri alisema kikosi cha Simba kimejipanga kuonyesha soka safi kwa sababu kinafahamu Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa wanayoshiriki ya Ligi ya Mabingwa Afrika yana ushindani na changamoto mbalimbali.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika kila mechi tutakayocheza, ushindani wa timu tunazokutana nazo, ushindani wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza pia unasababisha wachezaji wote kujituma, malengo yetu ni kufanya vizuri kwa kushinda mataji," alisema Phiri.

Mzambia huyo alisema pia alifurahi kuona amekamilisha usajili wa kujiunga na Simba kwa sababu klabu hii ni moja ya timu kongwe barani Afrika na kuitumikia ni sehemu ya heshima.

"Simba ni moja ya klabu kubwa Afrika, lakini pamoja na ukubwa wake, ina mashabiki ambao wanatupa ushirikiano mkubwa kiasi cha kutufanya wachezaji kuwa na furaha muda wote.

Wanatupa sapoti hata tunapocheza nje ya nchi, niliwaona nchini Malawi walikuja na ndani pia, muda wote na kila tunapokwenda na tupapopita wapo wanatushangilia, hii inatufanya wachezaji kuwa na furaha muda wote na kujiona tuna deni la kuwapa. Kwangu mimi binafsi nafurahishwa sana na nitajitahidi kufunga mabao ili wafurahi," alisema Phiri. Kuhusiana na majina ya vyeo vya kijeshi anavyopewa kama MP na Jenerali, alisema hamjui mtu aliyempa na anafikiri yametoka kwa mashabiki wa soka wanaomfuatilia kwa karibu.

"Huwezi kuwazuia mashabiki kukupa majina ambayo wao wanajisikia kukuita, lakini hata mimi nayasikia tu sijui ni nani aliyoyatoa kwangu, lakini kwangu mimi sina shaka, najisikia vizuri tu," alisema Phiri aliyesajiliwa msimu huu akitokea Zanaco ya Zambia.

Aliongeza Simba amepaona kama nyumbani kwa sababu alikutana na Mzambia mwenzake Clatous Chama, ambaye wanafahamiana siku nyingi na urafiki wao si uwanjani tu, hata nje ya uwanja na wa kifamilia.

Straika huyo ambaye ana mabao matatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mawili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, amewapongeza pia viongozi na benchi la ufundi la timu hiyo kwa wazo lao la kutafuta mechi za kirafiki katika kipindi hiki cha mapumziko kupisha Kalenda ya FIFA.

INAENDELEA UK 23

# Yanga SC yazichambua dakika 180 mechi za CAF

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha wanasonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamesema watakuwa makini katika dakika zote 180 watakazocheza dhidi ya wapinzani wao, Al Hilal ya Sudan.

Yanga itaikaribisha Al Hilal katika mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Oktoba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze alisema wachezaji wao wanatakiwa kubadilika ikiwa ni pamoja na kupambana kusaka mabao katika dakika tisini za mchezo wa kwanza.

Kaze alisema timu inapopata matokeo chanya katika mechi ya kwanza, husaidia kuondoa presha kwenye mchezo wa marudiano na hivyo kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele.

"Mara nyingi wachezaji wetu wanapoteza nafasi nyingi za wazi wanapokuwa wanashiriki michezo ya kimataifa, tunahitaji kuongeza umakini, ninamaanisha umakini unahitajika zaidi, mechi hizi za kimataifa ukiruhusu makosa, umekwisha," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema timu zote zina nafasi sawa ya kusonga mbele katika michuano hiyo na kinachotakiwa ni kuhakikisha wanajilinda pale watakapofanikiwa kupata mabao ya kuongoza.

"Mchezo uko sawa sawa, kwa pande zote mbili upo 50/50, kwa sababu timu ambayo watakutana nayo ina kiwango kizuri. Nimefanikiwa kuwafuatilia wapinzani wetu kupitia mchezo wao wa kwanza walioocheza nchini Ethiopia nikaona ni timu bora, tusipokuwa makini itatugharimu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa kuitaja Zalan FC ya Sudani Kusini, haikuwa bora ukilinganisha na kikosi chao, hivyo hawatakiwi kubweteka na matokeo ambayo waliyapata kwenye mechi zote mbili na kujipanga kujiimarisha.

"Tunajua mechi zote zitakuwa ngumu, lakini kama wachezaji watafuata maelekezo tutakayowapa, uwezo wa kutinga hatua ya makundi tunao, ni muda mrefu umepita tangu kucheza hatua hiyo, msimu huu tumeweka malengo ya kufika hatua hiyo," Kaze alisema.

Mrundi huyo aliongeza hata wapinzani wao, Al Hilal wanafahamu mechi zote mbili hazitakuwa rahisi kwa sababu ya kusaka matokeo bora.

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042